Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Tatu - Tarehe 4 Novemba, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

### Vyama vya Siasa

**MHE. USSI YAHAYA HAJI** aliuliza: -

Kwa kuwa Tanzania imekuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa tangu mwaka 1992, na kwa kuwa mfumo huo umewekewa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali ambazo chama cha siasa husika kinapaswa kufuata.

(a) Je, ni vyama vya siasa vingapi vimekaguliwa na kuonekana kuwa bado vinatimiza taratibu, kanuni na sheria za kuendelea na kuwepo kwa vyama hivyo vitajwa kwa majina?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa taarifa Bungeni kuhusu maendeleo ya vyama hivyo ili kuona kama vinatimiza masharti/taratibu, kanuni na sheria zilizowekwa au la?

(c) Iwapo kutakuwa na chama/vyama ambavyo vitabainika kukiuka sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa, je, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa dhidi ya vyama hivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mbunge wa Chaani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vyama vya siasa 16 vilikaguliwa na kuthibitika vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria, vinafuata masharti na taratibu zilizowekwa. Baadhi ya vyama hivi huwa na matatizo ya kiundeshaji na kiufundi, kisheria lakini yanarekebishika ambayo hayagusi uhalali wa usajili wake au kwa lazima kufutwa.

(b) Mheshimiwa Spika, taarifa kuhusu vyama vya siasa hutolewa katika hotuba ya Waziri Mkuu wakati wa Bunge la Bajeti kila mwaka. Taarifa hiyo inakuwa inajitosheleza kwa kuzungumzia masuala ya kuzingatiwa katika mfumo tulionao. Hii ni pamoja na maendeleo, matatizo ya kisheria na vyama vilivyofutwa kwa kupoteza sifa ya usajili au kukiuka sheria na hali ya kisiasa nchini

(c) Mheshimiwa Spika, endapo chama kitakiuka sheria, taratibu au kanuni, hatua zifatazo zitachukuliwa:-

(i) Msajili kukiandikia Chama barua ya kukitaka kujieleza kwa nini kisifutwe kwa mujibu wa kifungu cha 19 (2) sheria Na.5 ya mwaka 1992.

(ii) Msajili kutoa onyo la kawaida kwa Chama kilichobainika kukiuka sheria, taratibu na kanuni.

(iii) Msajili kufuta usajili wa Chama kwa mujibu wa kifungu hicho cha 19.

(iv) Msajili kusitisha kukipa ruzuku Chama kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha sheria Na. 5 ya mwaka 1992.

(v) Msajili kutoa taarifa Polisi ya kuitaka ichunguze matumizi ya ruzuku ya Chama na kuwashitaki viongozi mahakamani iwapo ataona na kuamini kuwa viongozi hao wametenda kosa la jinai kwa kutumia fedha za ruzuku vibaya.

(vi) Msajili kumshitaki kiongozi yoyote wa Chama mahakamani endapo atashindwa au kukataa kuwasilisha taarifa yoyote ya Chama kwa mujibu wa kanuni ya 13 na 16 ya kanuni za usajili.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Msajili anatekeleza kikamilifu jukumu lake na kuhakikisha kwamba vyama vya siasa hapa nchini vinafata taratibu, kanuni na sheria katika usajili na katika shughuli zake zote baada ya usajili.

**MHE. USSI YAHAYA HAJI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kupata majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa wapo baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wenye tabia ya kuhubiri udini, ukabila na maeneo na kwa kuwa wapo viongozi wa vyama vya siasa wanaosema hadharani kuwa vyama vyao visiposhinda nchi haitawaliki hasa kule Zanzibar.

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani ya kauli kama hiyo kinyume cha utaratibu na maadili ya nchi yetu na zinahashiria kuvuruga amani ya Taifa letu?

**SPIKA:** Usisome swali, kusoma swali ni kinyume cha taratibu. Lakini unaruhusiwa lijibiwe. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, vyama vya siasa vyote vinapaswa kufuata sheria Na. 5 ya vyama vya siasa na kanuni zake na Katiba ya nchi. Kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa masharti Na. 9 yanasema kwamba ni makosa kwa chama cha siasa kufanya yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chama hicho kinatetea na kupigania kuvunjika kwa Muungano ni makosa, Chama kinachotia udini au sehemu fulani ni makosa kwa hivyo vyama hivyo vinapaswa kufarakana even zinapoifuata hivyo msajili anahaki ya kufuta chama hicho cha siasa.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania ni moja katika nchi duniani zinazosifiwa kwa kuweka misingi mizuri ya demokrasia. Kwa kuwa sheria Na. 5 inasema vyama vya siasa pale inapotokea chama ambacho kinafanya vurugu kwa kuwa hakuna hatua zilizochukuliwa kikamilifu na mwandishi wa vyama hivyo na kwa kuwa ameviandika kumbe ametekeleza masharti, katika uendeshaji ikitokea matatizo hakuna hatua kama hizo, je, Wizara inaweza ikaleta sheria Na. 5 ili kuweka vyombo vya udhibiti kuhusu vyama vinavyoleta vurugu kwa sababu ni vyama vya siasa si vyama vya vurugu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kwa sasa hivi bado sheria hii ina nguvu zake za kutosha, haina haja ya sheria nyingine. La msingi ni kwamba viongozi hawa wa siasa lazima wafuate taratibu, kanuni na Katiba ya nchi na Msajili anao uwezo wa kufuta chama chochote cha siasa lakini Serikali yetu inajaribu sana kuvilea vyama vyetu hapa nchini kwa sababu bado vichanga.

Kwa hiyo, tuvipe nafasi tuvilee kwa sababu hiyo ndio kukua kwa demokrasia ya nchi yetu.

Na. 31

**Serikali katika Kutekeleza Miradi Mbalimbali**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza: -

Kwa kuwa maswali mengi huulizwa Bungeni kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali katika ngazi mbalimbali husika na kwa kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita nimeuliza maswali kadhaa juu ya mradi wa ujenzi wa daraja la Mto Bubu,

ukarabati kwa Bwawala Satched, ujenzi/ufunguzi wa vituo vya polisi vya Bashnet na Dareda, matatizo ya huduma za Mahakama za Mwanzo za Bashnet, Ufana na Dareda.

Je, Serikali imefikia hatua gani za dhati za utekelezaji wa miradi hiyo niliyoitaja pamoja na uondoaji/upunguzaji wa kero za Vituo vya Polisi na huduma za Mahakama?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa Daraja la Mto Bubu una umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya wananchi wa Wilaya ya Babati na Hanang ambako hicho ni kiungo katika eneo hilo kupitia sehemu ya Gidasi. Ujenzi ulitarajiwa kutumia mfuko wa barabara kwa makadirio ya shilingi milioni 75.0 kwa mwaka wa fedha 2003/2004/. Kutokana na ufinyu wa Bajeti, mradi huo ukawa haukutengewa fedha, kwa kuwa kiasi kidogo kilichopatikana kilielekezwa kwenye vipaumbele hususan barabara za mazao ya kilimo zilizotengewa shilingi 99,218,999.63.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Babati kujenga daraja la Mto Bubu bado iko pale pale licha ya kwamba fedha iliyopatikana kwa mwaka 2004/2005 kiasi cha shilingi milioni 168.0 pia hakikukidhi matarajio hivyo jitihada maalum zinafanywa na uongozi wa Wilaya ya Babati na Mkoa wa Manyara kuwasiliana na Mamlaka ya Mfuko wa Barabara *(RFB)* ili kupata fedha za kutekeleza mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Satched lilijengwa mwaka 1954 na lilikadiriwa kuwa na mita za ujazo 200,000. Ni kweli hivi sasa linahitaji ukarabati mkubwa kutokana na kujaa tope na mchanga unaoingia kutoka katika shughuli za kilimo zinazoendeshwa kandokando ya bwawa hilo. Nia ya Serikali ni kulifanyia ukarabati kwa kuondoa mchanga na kuzuia lisiendelee kujaa na hii itafanyika sambamba na kupiga marufuku shughuli zozote zinazowezesha kuendelea kuharibu mazingira na utunzaji wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa majengo ya Mahakama unatekelezwa chini ya mradi wa *Quick start.* Mikoa ya Arusha na Manyara imefanikiwa kuanza vizuri katika programu hii. Maeneo ya Bashnet, Ufana na Dareda katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge yatashughulikiwa mara ujenzi utakapokuwa unatekelezwa huko, lakini la muhimu ni wananchi kuendelea kuhamasishwa kuchangia nguvu zao ili kuboresha utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo cha Polisi Bashnet, uliangaliwa pamoja na ukarabati wa majengo ya mahakama. Lakini asasi hizi mbili hazitakiwi kuendesha ofisi zao ndani ya jengo moja. Kwa msingi huo kituo hakijaanzishwa. Kituo cha Dareda kadhalika kinahitajika, lakini ujenzi haujafanyika kutokana na hamasa ndogo ya nguvu za

wananchi kuchangia katika ujenzi wa kituo cha polisi. Hata hivyo Serikali inaendelea kuangalia njia bora zaidi ya kuwashirikisha wananchi katika kutekeleza mradi huo. Wananchi wanatakiwa kuonyesha dhamira yao ya kutaka kuwa na kituo hicho, kukijenga na baada ya hapo kuomba Serikali iwapeleke Askari pale ili kutekeleza majukumu yao ya kulinda wananchi/raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi wa Babati na Hanang kuona kwamba miradi hii ya huduma muhimu kwa jamii yetu inatekelezwa na kukamilika.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Naishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri lakini swali lenyewe la nyongeza. Je, kwa kuwa majibu haya yanayotolewa sasa hivi yalipaswa kuwa ndiyo mrejesho au *feedback* kwa muuliza swali kwa wakati mbalimbali lakini kwa nini au Serikali inachukua utaratibu gani au inatoa utaratibu gani wa kutoa maelezo ya hatua ambazo huwa zinafikiwa katika hoja kama hizo bila kusubiri Mbunge kuuliza tena swali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, miradi mingi inaazia Wilayani, kwa vyovyote vile au huombwa na Wilaya au Wilaya hushirikishwa katika kutekeleza miradi hiyo na kwa vyovyote vile naamini sasa Wilaya yenyewe inao uwezo wa kufuatilia ili kupata taarifa na ushirikishwaji unafanywa katika kutekeleza miradi hiyo kati ya sekta husika na Wilaya.

Kwa hiyo, kwa vyovyote vile kwa kuwa Wilaya inakaa vikao vya *full council,* Kamati za fedha na Kamati mbalimbali lazima taarifa hizi wanazo na sisi huwa tunawasiliana na Halmashauri na Mikoa kutoa taarifa hizi. Kwa hiyo, nina uhakika haya niliyoyasema akienda makao makuu ya Wilaya atapata hizi taarifa.

Na. 32

**Ukatili kwa Wanyama**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza: -

Kwa kuwa, katika miaka ya nyuma kulikuwepo na Chama cha *Tanganyika Society for Prevention of Cruelty of Animals (TSPCA )* ambacho kilisaidia sana kudhibiti ukatili kwa wanyama na kuwaheshimu viumbe hao kama ilivyo binadamu:-

(a) Je, Shirika hilo bado lipo ama limekufa kwa maana wanyama na ndege (kuku) hubebwa kwa ukatili mkubwa?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa wakulima wanaotumia wanyama kama ng'ombe na punda wakiwa wanawatesa sana hupata mavuno pungufu sana; na kama hivyo ndivyo, kwa nini wakulima hao wanaowatesa na kuwapiga ng'ombe na punda wanaolima hawachukuliwi hatua kama ilivyokuwa hapo zamani?

(c) Je, ni nani hasa anayetakiwa kuwapa msaada *(TPSCA)* ili wafanye kazi yao kwa ufasaha kama ilivyo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa wanyama pori?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Chama cha kuzuia ukatili wa wanyama yaani *TPSCA* kipo na kiliendesha shughuli zake vizuri zaidi miaka ya nyuma kama alivyoeleza Mheshimiwa Leonard Derefa. Kwa sasa chama hicho kutokana na muundo wake ni chama cha hiari na kwa hiyo, Wizara yangu haina mamlaka ya kusimamia uendeshaji wake isitoshe. Hivi sasa chama hicho kina kesi mahakamani.

Mheshimiwa Spika, upungufu uliojitokeza miaka ya hivi karibuni ni wanachama kutozingatia majukumu ya chama chao ya kuhamasisha vema jamii kuacha vitendo vya ukatili kwa wanyama. Hali ya kutokuwepo na uhamasishaji wa kutosha imewafanya watu wengi kudhani chama kimekufa na hivyo kuchochea ongezeko la vitendo vya ukatili kwa wanyama. Ili kunusuru wanyama na ukatili unaofanywa na baadhi ya watu ni wajibu wetu sote kukemea pale sheria zinazosimamia haki za wanyama zinapokiukwa. Chama hiki pekee hakiwezi kutekeleza juhudi za kupinga vitendo vya ukatili kwa wanyama.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya wakulima na wafugaji wanaotumia wanyama kama ng'ombe na punda kwa kilimo huwafanyia ukatili na hivyo kupunguza tija ya wanyama hao katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Huduma bora na lishe nzuri kwa wanyama kazi kwa hakika itawaongezea kipato bora wahusika. Kinyume chake wanyama wanapofanyiwa ukatili huumia na huchoka na hivyo kushindwa kufanya kazi. Pale inapothibitika kwamba mnyama amefanyiwa ukatili hatua za kisheria zichukuliwe kulingana na sheria ya kuzuia Ukatili wa Wanyama yaani *Animal Protection Ordinance.*

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa vyama vingine vya hiari ambavyo vinatekeleza majukumu yanayogusa jamii, sera na sheria za nchi, ni vyema chama hiki yaani *TPSCA* nacho kikajitafutia misaada ya kiutendaji inapobidi na Serikali daima itakuwa tayari kuweka mazingira ya kuwawezesha kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wasaidie juhudi za Serikali za kuimarisha vikundi vya jamii katika kutekeleza kazi zao na kuzingatia sheria za nchi ikiwemo sheria ya kuzuia ukatili wa wanyama.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa wa Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kusema kwamba *TSPCA* ni chama cha hiari lakini anakubaliana na mimi kwamba *TSPCA* imeazishwa na sheria ya Bunge la kikoloni yaani *Legical* mwaka 1951 na hivyo kuonekana chama cha Serikali na haoni wakati

umefika kwamba sheria ile ifutwe ili *TSPCA* na vyama vingine vya kulinda haki za wanyama viweze kuundwa upya?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwamba yeye ni mmoja wa wanachama wa *TSPCA* na katika uchaguzi uliopita yeye alikuwa mmoja wa wanachama walioshiriki katika kukiimarisha chama. Nakubaliana naye kwamba sheria ni ya zamani na inahitajika kutazamwa upya, lakini nadhani suala la msingi hapa ni kwamba chama kina matatizo na hivi sasa kipo mahakamani kwa hiyo kufanya lolote kabla hawajamaliza mgogoro wao kule mahakamani itakuwa vigumu.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Suala la wanyama na namna ya kuwaweka katika hali ya usalama ni la muhimu, sasa katika hili ningependa tu kufahamu majukumu ya Wizara kwa sababu vinavyosajiliwa pamoja na kwamba ni vyama vya hiari lazima kuna Wizara ambayo inavisimamia. Wizara ya Mifugo ina nafasi gani kwenye hili?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, jukumu la Wizara yangu ni kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha vyama hiari vyovyote vinavyosaidia mifugo viweze kuanzishwa.

Na. 33

**Maji-Kilema Kusini - Jimboni Vunjo**

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI** aliuliza: -

Kwa kuwa Kata ya Kilema Kaskazini-Jimbo la Vunjo imepakana na msitu mnene wa Mlima Kilimanjaro na kuna chemchem zaidi ya 12 zenye maji maangavu na mengi sana; na kwa kuwa kata ya Kilema Kusini, njia panda ya Himo na Chekereni haijapata maji ya bomba tangu tupate Uhuru na wakati wote huo wanaziona chemchem hizo za Kilema Kaskazini: -

(a) Je, Serikali hainoni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kufanya juhudi za makusudi kufikisha maji ya bomba la inchi 4 kwenye eneo la Kilema Kaskazini?

(b) Kama hakuna fedha za kutosha, je, Serikali iko tayari kutengeneza *in tanks* (vitega maji) kufikia eneo la kilometa 15 na hizo zilizobaki ziendelezwe kwa nguvu za wananchi kwa kusaidiana na mafundi wa Idara ya Maji na Wilaya ya Moshi?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kuendelea kuwategemea wahisani toka nje ya nchi kwa kila jambo ni kudumaza ari ya Serikali na hivyo kuwatesa wananchi wake tangu tupate Uhuru?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, naomba kutoa maelezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kilema ipo katika Tarafa ya Vunjo Magharibi na ina vijiji sita ambavyo ni Legho Mulo, Mrawe Kyura, Kilema Pofo, Kilema Chini, Masaera na Kilototoni. Eneo la njia panda ya Himo linajumuisha vijiji vya Kilema Pofo na Kilototoni. Chekereni ni kitongoji cha kijiji cha Ghona katika Kata ya Kahe Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo hayo yana maji ya uhakika. Huduma ya maji katika maeneo hayo ilikusudiwa kupatikana kutoka mradi wa maji wa Kilema katika awamu ya tatu na nne. Lakini kutokana na ukosefu wa fedha ni awamu mbili tu zilijengwa kwenye mradi uliobuniwa miaka ya 1970.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuwapatia maji wakazi wa Kilema Kaskazini. Katika kupunguza tatizo hili la maji, wananchi kwa kushirikiana na KKKT wamechimba visima virefu vinne eneo la Kilototoni na visima viwili vya pampu za mkono eneo la Chekereni na vyote vinatumika.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilitenga shilingi milioni 10 kwa ajili ya uchimbaji wa kisima kirefu kimoja eneo la njia panda ya Himo na tayari kisima hiki kimeshachimbwa na pampu imenunuliwa. Katika mwaka huu wa fedha 2004/2005 jumla ya shilingi milioni 15 zimetengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kukamilisha kazi zilizobaki ili huduma ianze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya Maendeleo *(KfV)* imekubali kugharamia usambazaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Moshi Vijijini. Kazi ya upembuzi yakinifu wa miradi imeanza tangu mwezi Machi, 2004 na inatarajiwa kukamilika Februari, 2005. Ujenzi wa miradi kwa awamu utaanza mwaka 2005/2006.

Upembuzi yakinifu wa miradi umebaini vyanzo vya maji vya Mshiri, Mue na Mae ambavyo vitatumika kuboresha hali ya maji katika maeneo yaliyotajwa pamoja na maeneo mengine.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanayapa matumaini Jimbo la Vunjo na maeneo husika kupata maji kama alivyomakini katika kututoshelezea maji katika nchi kama alivyofanya Mwanza na Shinyanga ikapata maji kutoka Ziwa Victoria.

**SPIKA:** Uliza swali basi.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, hali kadhalika nina imani sasa atatekeleza azimio lake nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ameridhika hana swali la kuuliza. *(Kicheko)*

Na. 34

**Mikopo kwa Vijana Waliohitimu Vyuo vya Ufundi**

**MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO** aliuliza: -

Kwa kuwa baadhi ya vijana wanaoshindwa kuendelea na masomo na sekondari hujiunga na vyuo mbalimbali vya ufundi kama *VETA* ili wapate mafunzo yatakayowawezesha kujiajiri wenyewe na hata kuajiriwa na kwa kuwa baada ya mafunzo hayo wengi hukosa ajira na hushindwa kujiajiri wenyewe kwa kukosa mitaji: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mikopo vijana hao ili waweze kujiajiri wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe wakiwemo wale wanaohitimu vyuo mbalimbali vya ufundi kama *VETA.* Moja kati ya hatua hizo ni uanzishwaji wa mfuko wa maendeleo ya vijana ambao lengo lake ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana ili kuanzisha na kuimarisha miradi yao mbalimbali ya kiuchumi.

Hadi sasa Serikali imeshatoa fedha za mikopo kwa ajili ya kuwaendeleza vijana kama ifuatavyo.

| **Mwaka** | **Kiasi** |
|---|---|
| 1994/1995 | 150,000,000/= |
| 1995/1996 | 150,000,000/= |
| 1997/1998 | 200,000,000/= |
| 1999/2000 | 100,000,000/= |
| 2000/2001 | 150,000,000/= |
| 2001/2002 | 372,800,000/= |
| 2002/2003 | 500,000,000/= |

Kwa hiyo, hadi kufikia mwaka 2003/2004 Serikali ilikwishatoa kiasi cha shilingi 1,622,800,000/= kwa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji kwa ajili ya kusaidia vikundi vya vijana waweze kuanzisha miradi mbalimbali huko waliko.

Aidha, Serikali imezielekeza Halmashauri zote za Wilaya na Mji kutenga 10% ya mapato yao kwa ajili ya mikopo kwa vijana na akina mama.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia hutoa mafunzo maalum ya stadi za kazi kwa vijana ikiwemo suala la matumizi bora ya mikopo. Mafunzo hayo huwapatia vijana ujuzi unaowawezesha kupangilia na kutumia vyema fedha za mikopo na hivyo kuendesha miradi yao kwa faida.

**MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Kutokana na hali hii ya utandawazi tunajukumu kama Serikali kuwawezesha vijana wetu kielimu, ufundi na kifedha lakini ukiangalia wanafunzi wetu wa darasa la saba na la kumi na mbili wanaoingia katika vyuo hivi ufundi idadi yao ni ndogo sana hailingani na wale wanaomaliza na wakashindwa kuendelea, wale wasiofaulu.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wakuongeza vyuo hivi vya ufundi kwa sababu kutokana na uhaba wa vyuo vya ufundi tulionao ndio maana ikawa idadi ya vijana wanaoingia katika vyuo vya ufundi ni ndogo na pia vilevile kutokana na uhaba wa fedha za kuwatoa vijana wao kutoka mikoani mpaka hapa.

**SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO:** Mheshimiwa Spika, je, kuna utaratibu gani au Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuongeza vyuo hivi vya ufundi katika kila Mkoa?

**SPIKA:** Sawa imeeleweka, una mpango gani Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba kila Mkoa kuna kuwa na Chuo cha *VETA.* Ndio maana mwaka huu wa fedha mikoa mitatu ambayo ilikuwa imebakia ya Lindi, Pwani na Manyara yote tunajenga vyuo vya *VETA* kimoja kila Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ningependa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba vyuo vya *VETA* madhumuni yake si kwa vijana waliomaliza darasa la saba na kushindwa kuendelea sekondari tu. Hata vijana wanaomaliza *form four, form six* na hivi sasa kuna watu wanaotoka Chuo Kikuu wanakuja kupata *praticals* za ufundi wao waliojifunza kule. Kwa hiyo, vyuo vya *VETA* ni vya wote.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii naomba niulize swali moja la nyongeza. Vijana wengi baada ya kumaliza mafunzo ya ufundi lengo la Serikali lilikuwa wajitegemee wenyewe lakini tatizo lililojitokeza vifaa vile vinakuwa bei mbaya sana katika maduka ya watu binafsi, je,

Serikali ina mpango gani ya kuwatafutia maduka ili waweze kununua kwa bei nafuu waweze kujitegemea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza lazima tukubaliane kwamba vijana hawa wanaokwenda kuchukua mafunzo ya ufundi si vijana wanaohitaji kulelewa kiasi hicho tunachofikiria. Wanapokuwa pale kwa vyuo hivyo hivi vya *VETA* kuna asilimia fulani ya vifaa vyao wanavyotengeneza hukatwa maalum kwa ajili ya kuwaandalia wanapotoka pale kama kikundi wawe na vyombo vya kuanzia. Tunachofanya Serikali ni kuongezea tu zile nguvu ambazo walikuwa wameshajiandalia. Kwa hiyo, sidhani kama kuna sababu ya kuandaa maduka maalum kwa ajili ya vijana wanaotoka katika vyuo vya *VETA* na vile vinavyofanana na vyuo vya *VETA*.

Na. 35

**Kero na Adha za Watoto Wasio na Makazi**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:

(a) Je, ni matatizo, kero au adha gani ambayo inaletwa na watoto wasio na makazi, ombaomba mitaani, ukosefu wa ajira kwa vijana mijini na vijijini?

(b) Je, Serikali ina mikakati na mipango gani kuondoa au kupunguza matatizo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Talala Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli watoto wasio na makazi, ombaomba, watoto wanaotembeza mmoja wa wazazi au ndugu kuombaomba mitaani, ukosefu wa ajira kwa vijana mijini na vijijini kunasababisha matatizo, kero na adha kwa watoto na vijana hao. Hii inatokana na ukweli kuwa watoto na vijana hao hukosa haki zao za msingi ambazo wanastahili kuzipata.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kupunguza matatizo, kero na adha wanazopata watoto na vijana hao Serikali inafanya mambo yafuatayo:-

(i) Wizara yangu imeandaa mwongozo wa Kitaifa wa malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi wenye misingi ya kijamii ili kushirikisha jamii katika suala zima la malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto hao.

(ii) Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* na Shirika la *Axios Foundation* inatekeleza mpango shiriki jamii wa

kuwatambua watoto walio katika mazingira magumu zaidi kwa lengo la kushirikisha jamii na wadau mbalimbali katika suala la kuwahudumia watoto hao. Mpango huu tayari umeshaanza kutekelezwa katika Halmashauri za Wilaya 19 ambazo ni Bagomoyo, Kisarawe, Magu, Makete, Karagwe, Musoma Vijijini, Bunda, Jiji la Mwanza, Masasi, Mtwara Mikindani, Singida Vijijini, Singida Mjini, Ngara, Kibondo, Manispaa ya Mbeya, Rungwe, Muheza na Temeke.

(iii) Katika kutekeleza mpango huu watoto wanaotambuliwa kuwa wana umri wa kuanza shule na hawajaandikishwa shule za msingi au katika madarasa ya MEMKWA kwa wale ambao wamevuka umri wa kuandikishwa shule. Jamii na wadau mbalimbali hushiriki katika kuwapatia watoto hao huduma mbalimbali muhimu kwa ajili ya malezi, matunzo na ulinzi.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali ya niongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa watoto wa mitaani, ombaomba na vijana wanaokosa ajira wengi wao chimbuko lao kubwa ni vijijini.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuelekeza nguvu zake zote vijijni kama njia ya kusitisha hali hiyo ya sasa kuendelea?

(b) Je, Serikali inaweza basi ikaeleza mikakati maalum na misaada yake kwa Serikali za vijiji ili kuweza kupambana na hali hiyo huko vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu mswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli chimbuko la watoto ombaomba sehemu kubwa linatokea vijijini na kwa maana hiyo tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya kuelekeza nguvu za Serikali na mikakati mbalimbali huko vijijini na ndilo jambo linalofanyika hivi sasa, moja kuyarudisha yale madaraka kule vijijini.

Lakini pili, huduma za msingi za jamii za shule, barabara za vijijini, maji na afya ndio moja ya sehemu ya kurudisha huduma hizi muhimu vijijini ambazo vijana wengi wanafikiri ziko mijini tu lakini wakija hawazikuti. Kwa bahati mbaya wanaziona kwa macho. Kwa hiyo, nafikiri ushauri wake alioutoa ndio unatekelezwa na Serikali hivi sasa.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mtindo wa kuwatumia watoto wadogo katika shughuli za ombaomba una athari kubwa sana kwa watoto wanaohusika kwa kuwanyima haki yao ya msingi ya kwenda shule na vilevile kuwajengea fikra kwamba ombaomba ni mtindo wa maisha ambao hata nao wakikua wanaweza kujihusisha nao.

Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuleta sheria haraka iwezekanavyo katika Bunge hili ili iwe ni marufuku kuwatumia watoto wadogo katika shughuli za ombaomba?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Tunakubaliana na yeye kama tulivyoonyesha katika jibu la swali la msingi kwamba kutumika kwa watoto hawa wadogo kuwaongoza ombaomba kunawanyima haki zao za msingi.

Lakini tunafikiria si vyema kutanguliza sheria kabla ya elimu na utafiti wa kutosha ndio maana tumesema Serikali kwa kushirikiana na *UNICEF* na *Axios Foundation* tunafanya utafiti, lakini vilevile tunakusanya kumbukumbu sahihi kwa kushirikisha jamii ili itakapotungwa sheria kila mwanajamii atambue wajibu wake kwanza. Maana kwa kweli lazima tukubaliane kwamba sisi kama jamii tuna jukumu kubwa kabisa la kupunguza kadhia hii inayowakuta watoto wetu kuwaongoza ndugu zetu kaka zetu, binamu zetu, shangazi zetu katika ombaomba mijini.

Na. 36

**Umeme Utokanao na Mradi wa *Mnazi Bay***

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Bunge la Bajeti, 2004/2005 Serikali ilieleza kuwa Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara iendelee kusubiri utafiti wa umeme wa *Mnazi Bay* badala ya kutumia umeme wa *Songas* ulio tayari kutumika.

(a) Je, kwa nini Mikoa ya Lindi na Mtwara iendelee kusubiri utafiti wa umeme wa *Mnazi Bay* badala ya kutumia umeme wa *Songas* ulio tayari kutumika?

(b) Je, ni lini hasa mradi wa umeme wa *Mnazi Bay* utakamilika na ni hatua gani imefikia hadi sasa?

(c) Je, ni mradi upi utatumika kupeleka umeme wa uhakika kwenye Wilaya ya Liwale ambayo iko umbali wa kilometa 230 kutoka Songo Songo na umbali wa kilometa 430 kutoka *Mnazi Bay* na unapita vijiji gani hadi kufika Liwale?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali kikamilifu la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumekwisha eleza mara nyingi hapa Bungeni, ili kupitia umeme mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kutumia gesi ya Songo Songo zinahitajika karibu ya shilingi za bilioni 40 na kama ambavyo tulishawahi kusema uwekezaji katika eneo hili ulikuwa haukupatikana.

Mheshimiwa Spika, mtambo wa kuzalisha umeme wa njia ya gesi asilia ya Songo Songo utakaofaungwa Somango Fungu katika mradi wa *Songo Songo Wayleave Village Electrification Scheme* una wezo wa *5 MW* tu. Uwezo huu pia ni mdogo na hivyo hauwezi kutumika kupeleka umeme katika eneo lililo umbali wa kilometa 230 hadi Liwale. Pamoja na maelezo hayo, laini itakayojengwa kutoka Somanga Fungu hadi Singino (Kilwa Masoko) ni ya kilovoti 33 ambayo kitaalamu haiwezi kutumika pia kupeleka umeme umbali wa kilometa 230 kwa kuwa umeme utakaofika huko utakuwa hauna ubora unaofaa *(low voltage)* na hivyo kutoweza kutumika kwa shughuli nyingi au shughuli muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Mtwara na Lindi ipo gridi ndogo ya mtandao wa umeme wa kilovoti 33 ambayo unasafirisha umeme kutoka vituo vya kuzalisha umeme vya Mtwara, Lindi na Masasi hadi Nachingwea. Kwenye masuala umeme Liwale ipo umbali wa kilometa zaidi kidogo 100 tu kutoka Nachingwea ambapo umeme wa gridi hiyo ndogo unaishia na siyo kilometa 450 kutoka Mtwara ambapo umeme wa *Mnazi Bay* utazalishwa. Kutoka Nachingwea laini ya umeme wa kilovoti 33 inaweza kujengwa kwenda Liwale umbali wa kilometa kama nilivyosema awali zaidi kidogo ya 100 ambapo gharama yake itakuwa ya chini kuliko ile ambavyo ingetokea vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kazi inayofanyika hivi sasa na wawekezaji wa *Artumas* Kampuni inayotoka Canada ni kutathmini kiasi cha gesi iliyopo katika kisima cha gesi kilichopo *Mnazi Bay.* Mara baada ya kuridhika kuwa kuna gesi ya kutosha, mwekezaji ataendeleza mradi na kuzalisha umeme wa kiasi cha megawati 15 kwa ajili ya matumizi ya mikoa ya Mtwara na Lindi na baadaye Tunduru. Kazi ya kutathmini kiasi cha gesi iliyopo inatarajiwa kuchukua miezi sita kuanzia Julai, 2004 na awamu ya pili itajengwa kwa mwaka mmoja utakaoishia Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kurudia kauli ambayo tulishawahi kuitoa wakati wa Bunge la Bajeti kuwa Serikali ina matumaini makubwa kuwa mradi huu wa *Mnazi Bay* utafanikiwa. Hata hivyo, endapo majibu ya uhakiki wa gesi iliyopo *Mnazi Bay* hayataridhisha, Serikali inakusudia na inajiandaa kutumia utaratibu mwingine wa kuwezesha umeme wa uhakika kunapatikana katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Nashukuru kwa kupata majibu hayo mazuri lakini nina maswali mawili ya niongeza. Kwa kuwa sasa hivi Liwale unapata umeme wa jenereta ambayo ni *KW 200* tu na matumizi ya Liwale inazidi *KW 320.*

(i) Je, ni vipi Serikali itaboresha umeme wa Liwale ili uweze kutumika vile vile katika mitandao ya simu ambayo hivi sasa wako karibu kufungua huko Liwale?

(ii) Mimi nina habari za uhakika kabisa kwamba Liwale haitaweza kupatiwa umeme wa gridi wala huo kutoka Nachingwea, kwa kuwa hata Meneja wa *TANESCO* wa Liwale haudhurii tena vikao ambavyo vinaweza kurahisisha uletaji wa umeme wa kutoka *Mnazi Bay* wala *Songas.*

**SPIKA:** Hebu uliza swali usiweke maelezo marefu.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Kwa vile kuna ukweli kwamba sasa hivi Liwale haitapatiwa umeme wa *Songas* au *Mnazi Bay,* je, Serikali itafanya mpango gani wa kuendelea kuboresha umeme huo uwe wa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana nae kwamba kuna upungufu wa uzalishaji wa umeme pale Liwale. Liwale kuna mashine mbili zinazozalisha umeme kila moja yenye uwezo wa *KW 200* na kama mashine hizi zote zingefanya kazi kwa ukamilifu mahitaji ya umeme wa Liwale yangekuwa yamekamilika. Sasa hivi moja ya mashine hizi ina matatizo na inahitaji matengenezo makubwa, lakini inafanyakazi pale tu panapokuwa hakuna njia nyingine. Kwa hiyo, mashine ambayo inafanyakazi moja kwa moja ni moja na kwa ajili hiyo kuna masaa ambayo umeme huzimwa karibuni kwa saa kama nne kwa siku katika saa 24 ili kuhakikisha kwamba mashine ile inayofanyakazi pia inapata muda wa kupoozwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *TANESCO* inafanya juhudi ya kufanya matengenezo ya mashine hii nyingine ili umeme uendelee kupatikana kwa uhakika zaidi.

Kuhusu Liwale kwamba ana uhakika Mheshimiwa Mbunge kwamba haitapata umeme ama wa *Mnazi Bay* au wa Songo Songo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na kupitia kwake kuwahakikishia wananchi wa Liwale kwamba kauli ya Serikali inayohusu umeme wa Liwale kutoka kwenye mradi wa *Mnazi Bay* endapo utafanikiwa ni kauli thabiti na hakuna shaka kwamba katika kutekeleza mradi huu umeme wa Liwale utaunganishwa kutoka Nachingwea endapo mradi huu wa *Mnazi Bay* utafanikiwa.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa kwenye jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Serikali bado haina uhakika kuhusu kiwango cha gesi katika mashimo ya *Mnazi Bay,* lakini Serikali haipingi kwamba gesi ya Songo Songo ipo ya kutosha ambayo inaweza kupeleka umeme Lindi na Mtwara.

Je, ni jambo gani ambalo Serikali imefanya ione shida kutumia gesi ya Songo Songo kupeleka umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hata katika kikao cha Bajeti, swali la mwisho ambalo tulilijibu kuhusu umeme wa Mtwara na Lindi lilikuwa swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, juu ya umeme huu unaotokana na gesi ya Songo Songo au *Mnazi Bay.*

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia kwamba Serikali haioni ugumu kuwapatia umeme wananchi wa Mikoa ile kwa kukataa tu. Tulishaeleza hapa Bungeni na napenda nirudie kwamba ukweli ni kwamba haukupatikana uwekezaji wa kuweza kufikisha umeme katika Mikoa hii kupitia mradi wa Songo Songo na ndio maana Serikali ilipopata uwekezaji kupitia gesi ya *Mnazi Bay* ilikaribisha uwekezaji huu na inaendelea kushirikiana na wawekezaji hao kuhakikisha kwamba Mikoa hii miwili inapata umeme wa uhakika. Kama nilivyosema endapo kutatokea tatizo ambalo hatulitarajii Serikali itatafuta njia nyingine.

Na. 37

**Mapato Yatokanayo na Madini**

**MHE. TEMBE K. NYABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu kuanza kwa uchimbaji wa madini kama dhahabu katika migodi mikubwa ya Geita, Kahama, Nzega, Nyamongo, Buhemba na *Tanzanite* Merelani, Serikali ilitarajia kupata mapato.

(a) Je, Serikali imepata fedha kiasi gani kama mrabaha kutoka katika kila mgodi mmoja mmoja niliotaja na jumla ya Pato la Taifa kwa kila mwaka tangu uchimbaji huo uanze hadi sasa?

(b) Je, mapato hayo yatokanayo na madini ni asilimia ngapi ya pato lote la Taifa?

(c) Je, ni sekta ipi inaongoza kwa kuchangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa letu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tembe K. Nyaburi, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *Geita Gold Mine* ilianza uzalishaji mwezi Agosti, 2000. Hadi Desemba, 2003 mgodi huo ulilipa mrabaha wa jumla ya *US$18.2 million.* Mgodi wa Bulyanhulu unaomilikiwa na *Kahama Mining Corporation Limited* ulianza uzalishaji mwezi Julai, 2001. Hadi mwaka 2003 mwishoni ulilipa mrabaha *US$6.5 million.* Mgodi wa *Golden Pride,* Nzega umekuwa ukizalisha dhahabu tangu Februari, 1998 ambapo hadi Desemba, 2003 ulishalipa mrabaha jumla ya *US$7.2 million.* Mgodi wa *North Mara* uliopo Nyamongo ulianza uzalishaji mwezi Agosti, 2002 hadi Desemba, 2003 ulishalipa

Serikalini mrabaha *US$2.7 million. Buhemba Gold Mine* ilianza uzalishaji Februari, 2003 na hadi Desemba, 2003 ulishalipa mrabaha wa *US$ 778,750.*

Aidha, mgodi wa *Tanzanite* wa Mererani, *Mererani Mining Limited* ulianza rasmi uzalishaji mwaka 2000 hadi kufikia Desemba, 2003 mgodi huo ulishalipa jumla ya *US$ 361,000* kama mrabaha . Jumla ya Pato la Taifa kwa kila mwaka tangu uchimbaji huo uanze ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1998 mrabaha *US$ 0.5 million* na kodi nyingine *US$1.7 million,* mwaka 1999 mrabaha *US$ 1.2 million* na kodi nyingine *US$ 3.7 million,* mwaka 2000 mrabaha *US$ 4.7 million* na kodi nyingine *US$ 14.3 million,* mwaka 2001 mrahaba *US$ 7.1 million* na kodi nyingine *US$ 17.4 million,* mwaka 2002 mrabaha *US$ 10.9 million* na kodi nyingine *US$ 23 million* na mwaka 2003 mrabaha *US$ 16.5* na kodi nyingine *US$ 27.3.*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa mapato yanayotokana na madini yanachangia wastani wa 3% katika Pato la Taifa.

(c) Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ndiyo inayoongoza katika kuchangia katika Pato la Taifa ambapo kwa mujibu wa taarifa tulizokuwa nazo inachangia zaidi ya asilimia 45 kwa bei za sasa kwa mujibu wa kitabu cha Hali ya Uchumi kilichotolewa mwezi Juni, 2004 na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Mchango huo ni 46.8% kwa bei za mwaka 1992.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kiwango cha mrabaha ambacho kinalipwa ni asilimia 3 na katika nchi nyingi kiwango cha mrabaha ni kati ya asilimia 3 mpaka 8, sasa je, Serikali ina mpango gani wa kuona kwamba kiwango hiki kinapandishwa ili kioane na hali halisi ya madini yanavyozidi kuchimbwa hapa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niliharifu Bunge lako Tukufu kwamba hiki kiwango cha mrabaha na vya kodi vimepatikana kutokana na tafiti mbalimbali zilizofanywa na Serikali katika nchi mbalimbali ambazo zinazalisha madini. Lakini hata hivyo Serikali inatambua kwamba suala la mrabaha limekuwa ni jambo ambalo limezungumzwa sana katika Bunge hili ni kutokana na kuelewa hivyo kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, alishaunda Tume za kuchunguza masuala yote yanayohusu madini kwa madhumuni ya kutathmini kiasi gani Taifa linapata na namna gani mapato haya yanaweza kuboreshwa zaidi kwa ajili ya nchi yetu.

Tume hii hivi sasa inakusanya taarifa mbalimbali ambazo imezipata na katika muda muafaka naamini kabisa watawasilisha taarifa hii kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu

ili kuweza kujua tunafanyaje sasa katika suala la madini ikiwa ni pamoja suala la mrabaha kama itaonekana kwamba inabidi litazamwe upya.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu la (c) Mheshimiwa Naibu Waziri, amekubali kwamba kilimo ndicho kinaongoza kwa kuchangia Pato la Taifa.

Je, Serikali inatoa kiasi gani cha fedha zake ili kukiendeleza kilimo katika nchi hii ya Tanzania?

**SPIKA:** Naona Mawaziri wanashauriana kwanza. Mawaziri wananiambia kuwa hilo ni swali jipya kwa hiyo, lazima watafute majibu ya kuridhisha.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa ya nafasi kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mikataba na sheria ya madini iliyopo sasa hivi imeonekana ina mapungufu na hivyo kupelekea nchi yetu kuporwa raslimali hizo na kwa kuwa Serikali imelitambua hilo ndio maana imeunda Tume ya kuangalia upya sheria ya madini kazi ambayo haijakamilika.

Je, Serikali itakubaliana na mimi sasa isitishe kusaini mikataba mipya ya madini hadi hapo sheria itakapokuja kufanyiwa marekebisho?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Musalika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kupata wawekezaji katika sekta ya madini ni suala lenye ushindani mkubwa duniani, nchi yetu imebahatika kuweza kupata wawekezaji hawa ambao tumewapata na wengine tunawakaribisha. Kwa hiyo, kwa wakati ambapo Serikali inaendelea kutathmini sekta hii ya madini kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameunda Tume, isingekuwa busara kufunga milango kwenye suala la uwekezaji katika sekta hii ya madini ambayo ni sekta muhimu kama unavyofahamu katika uchumi wetu ambayo ni sekta pia ambayo ina ushindani mkubwa katika kuhakikisha kwamba tunapata mitaji iliyopo hapa duniani.

Na. 38

**Utekelezaji wa Mkataba wa Serikali na Mwekezaji katika *TTCL***

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa, baada ya mgogoro wa malipo ya *USD* 60,000,000 kukamilika kati ya Serikali na mwekezaji katika Kampuni ya Simu *(TTCL):-*

(a) Je, ni mipango gani imeanza kutekelezwa na Kampuni hiyo kufuatana na mkataba wa awali wa utendaji kama vile kuongeza idadi ya simu kufikia 810,000 kutoka 200 zilizokuwepo?

(b) Je, Kampuni imeshalipa deni la faini waliyopewa na Tume ya Taifa ya Mawasiliano la *USD* 44,000,000 kutokana na kushindwa kutekeleza matakwa ya mkataba?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali kama zifuatazo:-

(a) (i) Kuimarisha na kuongeza njia kuu. Hizi zikiwemo za Nyororo - Songea, Kaluwe - Sumbawanga - Nkasi. Dar es Salaam *(optic fibre ring)* ambayo inaanzia Ali Hassan Mwinyi-Kijitonyama-Ubungo-Magomeni-*Pugu Road*-Kurasini na kuunga tena Dar es Salaam. Uimarishaji wa uongezaji wa njia kuu hizi umewezesha makampuni ya simu za mikononi kufikisha mitandao yao katika maeneo husika.

(ii) Kuondosha mitambo ya *analogue* na kuweka ile ya *digital* katika maeneo yafuatayo:-

Mafinga, Makete, Ludewa, Maswa, Tunduma, Meatu, Sengerema, Nansio, Kibondo, Kasulu, Pangani, Mufindi, Manyoni na Karagwe. Pia imekamilisha katika maeneo ya Kiomboi na Namanyere hivi karibuni. *TTCL* iko mbioni kuweka *digital link* toka Dar es Salaam kwenda Mtwara. Tunategemea *TTCL* ikamilishapo *link* hii miji ifuatayo nayo itapata huduma za mawasiliano ya kisasa. Miji hiyo ni Mkuranga, Kibiti, Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Ikwiriri, Utete, Mafia, Nangurukuru, Lindi na Mtwara.

(iii) Utoaji wa huduma za simu za mkononi, ambapo kampuni ya *Celtel* imeweza kusambaza huduma zake takriban mikoa yote.

(iv) Uanzishwaji wa *prepaid services* katika mikoa yote.

(b) Mheshimiwa Spika, upo uhusiano kati ya uenezaji wa mtandao na utoaji wa faini pale uenezaji unapokuwa haukukamilishwa. Lakini mkataba pia unaeleza ni pale tu penye faida ndipo kigezo hiki cha faini kinatumika.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa matumizi ya simu ya mkononi kumepunguza kasi ya maendeleo ya simu za msingi. Hii si kwa Tanzania tu bali ni duniani kote. Kwa mfano, uwezo wa Kampuni ya simu Tanzania ni *line 250* lakini

watumiaji halisi wa mtandao huu ni 154,000 tu. Hivyo ipo haja ya kutazama upya suala la huduma badala ya kufikiria nambari. Hata hivyo suala zima la faini.

Mheshimiwa Spika, linashughulikiwa na Mamlaka ya Mawasiliano kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa hapo awali.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sasa hivi kuna mgogoro wa watumishi wa *TTCL* na *management* na moja ya sababu ya mgogoro huo ni kushindwa kutekelezeka kwa mkataba huu maana upanuzi haukwenda kama ilivyotarajiwa. Je, Serikali inakubaliana nami kwamba wafanyakazi kwa sababu sio kosa lao wanahaki ya kulipwa *a golden hand shake* nzuri ili waondoke vizuri?

Je, Serikali inakubaliana nami kwamba kutumia zile dola milioni 60 dola kuanzisha shughuli za *Celtel* ni kinyume cha makubaliano ya mkataba wa awali na ndio chimbuko la matatizo ya *TTCL* leo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Henry Shekiffu, kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema katika swali lake la kwanza kwamba wafanyakazi wamepeleka malalamiko yao mahakamani, naomba niseme sipendi nilizungumzie hili kwa sababu masuala haya yako mahakamani tuache mahakama iamue.

La pili ni kweli dola milioni 60 kwa makubaliano zilitumika kutengeneza simu za *Celtel* lakini nakubali kwamba masuala haya yako katika mjadala hivi sasa ni namna gani fedha hizi zinaweza kurudi katika *TTCL* kufanya *TTCL.*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali la niongeza. Katika mpango wa *TTCL* kuweka mitambo mipya ilikuwa imetoa ahadi kwamba katika kuweka mtambo mpya katika mji Kiomboi utakaofuatia ni mji mdogo wa Itigi. Lakini katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba Kiomboi ametaja miongoni mwa miji ambayo imekwishawekewa mitambo mipya na miji inayofuata lakini mji wa Itigi haupo.

Je, ndio kusema kwamba Wizara imekiuka ahadi yake ambayo ilikuwa imetoa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama atakumbuka Mheshimiwa Ismail Iwvatta, hapo awali tulikuwa na mpango wa kuondosha mtambo wa Manyoni ili ukafanye kazi kule Itigi na

tukaweka mtambo mpya Manyoni kwa lengo la kuboresha mawasiliano ya simu Manyoni. Lakini ni bahati mbaya mtambo ule haukuweza kuingiliana na mitambo mingine kwa maana hiyo ukawa haufai kwenda Itigi. Lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama tuliahidi kupeleka simu kule kwake tutahakikisha kwamba simu zinafika.

Na. 39

**Huduma ya Simu - Mhunze**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. PAUL N. MAKOLO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilitamka kuwa utafanyika utafiti ili kuona uwezekano wa kuweka simu katika mji wa Mhunze ambao ni makao makuu ya Wilaya ya Kishapu:-

Je, ni nini matokeo ya utafiti huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Utafiti *(Survey)* katika kuangalia mahitaji halisi ya huduma ya simu hapo Mhunze bado haujakamilika. Hata hivyo, kampuni ya simu ina nia thabiti ya kupeleka simu za kisasa pamoja na simu za vibandani kwenye miji midogo na vijiji vyenye mwelekeo wa kibiashara lakini utekelezaji wake unakwama kutokana na uhaba wa fedha.

Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa kupeleka huduma ya simu za kisasa vijijini nchini kote, Serikali, ina mpango wa kuanzisha mfuko maalum ujulikanao kama *Universal Access Fund,* kwa ajili hiyo wadau mbalimbali watahusishwa katika kuchangia mfuko huo na ni mategemeo yetu kuwa mara mfuko huo utakapoanza kutumika, tatizo la ukosekanaji wa huduma za simu za kisasa vijijini litapungua kwa kiasi kikubwa.

**MHE. MGANA M. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu mpaka sasa inaonyesha kwamba *TTCL* ina ugumu wa kutoa huduma za simu.

Je, Waziri atakubaliana nami kwamba sasa upo umuhimu wa kuwahimiza watu kama *Celtel* na *Vodacom* waweke simu kwenye vijiji ambavyo vilikuwa vipate simu za *TTCL* zikiwepo Mhunze, Kongi na kwinginepo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la niongeza la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana nae kuwa tumesuasua kidogo katika masuala ya kampuni ya simu kuendeleza huduma ni kutokana na migongano ambayo ilikuwepo hapo awali. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi tunawahimiza sana wawekezaji wetu wa simu za mikononi pale inapowezekana wafike katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba nichukue nafasi hii niwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wengi wamepata mawasiliano ya simu za mikononi katika maeneo yao hii ni dalili tosha kwamba Serikali inajali matatizo ya wananchi wake na tutaendelea kufanya hivyo.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Kwa kuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali nyingi za kupeleka simu sehemu mbalimbali na nyingi zimetekelezeka; na kwa kuwa suala la kusambaza simu ni suala linalohusu sera ya Chama Tawala na kwa kuwa katika Wilaya ya Kilolo ahadi alizotoa kupeleka simu Kilolo - Ilula tayari imeanza kufanyiwa kazi.

Je, Waziri atakuwa tayari kuja kuhudhuria katika uzinduzi wa shughuli hiyo kwa sababu ni suala ambalo linagusa wananchi wengi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waziri yuko tayari kuja kuhudhuria, tunaendelea na maswali kwa Wizari ya Sheria na Mambo ya Katiba. Mheshimiwa Karim Said Othman. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 40

**Sheria ya Ubakaji**

**MHE. KARIM SAID OTHMAN** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna sheria inayowabana watu wenye tabia ya ubakaji; na kwa kuwa watu wengine hubaka kwa sababu mbalimbali zikiwemo imani za kichawi, tamaa za kimwili na wengine hubaka kwa makusudi wakijua kabisa kuwa ni waathirika wa UKIMWI na lengo lao ni kuwaambukiza wengine na wanaobakwa hubaki na aibu, huathirika kisaikolojia, kashfa, majeraha na magonjwa kama UKIMWI.

(a) Je, Serikali inaona sheria na hukumu iliyopo kwa sasa inatosha kukidhi haja ya makosa hayo?

(b) Kama haitoshi, je, kwa nini Serikali isitunge sheria nyingine kali zaidi ambayo inamhukumu mhalifu ambaye ni mwathirika kama mtu aliyeua kwa makusudi?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Karim Said Othman, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) , (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa lengo la kudhibiti vitendo vya ubakaji, mwaka 1998 Serikali iliwasilisha Bungeni, Muswada wa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana yaani *the Sexual Offences Special Provisions Act, 1998.* Bunge lilipitisha Muswada huo na sasa ni moja kati ya Sheria zinazotumika katika kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa wanawake.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, mtu anayepatikana na hatia kwa kosa la kubaka adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30 na kisichozidi kifungo cha maisha pamoja na viboko. Endapo wakati wa kutenda kosa la kubaka, mtuhumiwa atasababisha majeraha kwa aliyembaka, atatakiwa pia kumlipa fidia muathirika. Serikali inaona adhabu hiyo ni kali na inakidhi haja ya kutoa adhabu inayolingana na makosa hayo.

(b) Kama nilivyosema katika jibu la sehemu (a), adhabu iliyopo inatosha na Serikali haioni sababu ya kufanya marekebisho katika sheria hiyo kwa sasa. Pendekezo la kumwadhibu mtuhumiwa ambaye ni mwathirika wa UKIMWI kama mtu aliyeua kwa makusudi linazungumzika na Serikali imepokea ushauri na itaendelea kulifikiria.

Hata hivyo, misingi ya sheria za makosa ya jinai inahitaji kuwepo mtu aliyefariki kutokana na vitendo vya mtuhumiwa ili kuweza kumweka hatiani mhalifu. Mtu aliyebakwa na mtu mwenye UKIMWI hafi wakati kitendo hicho kinapofanyika. Mtu aliyebakwa anaweza kuendelea kuishi kwa muda mrefu kabla ya dalili za kuathirika hazijatokeza na hivyo kuwa vigumu sana kuthibitisha kosa la mauaji. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimwa Spika, kwa kuwa Tanzania nayo iko katika ulimwengu huu tuliyokuwa tunaishi, na kwa kuwa nchi nyingi ulimwenguni bado zinaendelea na hukumu au adhabu ya kifo hata kwa makosa ya kupatikana na madawa ya kulevya. Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuwa ni wakati muafaka kwamba hawa wabakaji ambao wanawadhalilisha watoto wadogo na akina mama watapewa adhabu ya kifo ili wale wanaobakwa wajihisi starehe ndani ya ulimwengu huu. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza inaniwia vigumu kwa mwezi huu wa Ramadhan kujibu maswali haya ya ubakaji, inakuwa ni vigumu kwa kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini la pili ni kusema kwamba masuala haya ya ubakaji ni afadhali tu wananchi kwa kweli badala ya kujihusiha na masuala ya ubakaji, waseme nao. Waendelee kusema

nao badala ya kujihusisha na masuala ya ubakaji. Baada ya kusema hayo niseme tu kwamba ukifanya hivyo kweli utakuwa unakwenda kinyume na maazimio ya Kimataifa. Kumnyonga mtu kwa sababu hiyo, itakuwa tu kwa kweli ni kumdhalilisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninachosema kwamba utakuwa unakwenda kinyume cha utaratibu ama sheria au mikataba ambayo tunayo hapa duniani.

**SPIKA:** Tumuonee huruma Waziri, tuachane na maswali ya ubakaji wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 41

**Dua ya Mahakama Isomwe Bungeni.**

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU** aliuliza:-

Kwa kuwa, utawala wa Tanzania una mihimili mikuu ambayo ni Bunge, Serikali na Mahakama; na kwa kuwa vikao vya Bunge huanza kwa kusoma Dua ya kuiombea Serikali na Bunge.

(a) Je, kwa kufanya hivyo si kuvunja Katiba ya nchi yetu?

(b) Ni lini Dua ya kuiombea Mahakama itaanza kusomwa Bungeni ili kurekebisha uvunjaji huo wa Katiba?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kabla ya kuanza shughuli zake kila asubuhi, Bunge linaomba Dua kuliombea Bunge, Rais na Serikali. Katika Dua hiyo, Mahakama haitajwi. Hali hii inatokana na muundo wa Bunge ambao unaojumuisha shughuli za Bunge na za Serikali. Mawaziri wa Serikali ni sehemu ya Bunge kwa sababu wanateuliwa kutokana miongoni mwa Wabunge.

Kwa kuwa Mahakama siyo sehemu ya Bunge ndiyo maana hawawakilishwi Bungeni, kwa mantiki hiyo, Bunge halivunji Katiba kwa kutoitaja Mahakama wakati dua inaposomwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Mahakama hautoi fursa kwa watendaji wake yaani Majaji na Mahakimu, kuomba Dua kwa pamoja kama inavyofanywa Bungeni. Mahakama imetenga Siku ya Sheria inayoadhimishwa nchini kila mwaka kuashiria

kuanza kwa vikao vya Mahakama. Siku ya Sheria huadhimishwa kwa gwaride la askari na Dua kutoka kwa viongozi wa Dini. Serikali inaamini kuwa utaratibu huu kwa sasa unatosha.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, kwamba Katiba haina sharti lolote kuhusu kuombea Bunge, Serikali wala Mahakama. Hivyo, si sahihi kusema kwamba Bunge huvunja Katiba kwa sababu ya kutotaja Mahakama wakati wa Dua ya kuliombea Bunge.

Na. 42

**Barabara ya Mjini Mugumu - *Fort Ikoma* (Kilometa 30)**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Mjini Mugumu hadi *Fort Ikoma* ni muhimu sana kwa wananchi wanaosafiri toka Mjini Mugumu kwenda Arusha kupitia Hifadhi za Serengeti; na kwa kuwa barabara hii mara nyingi iko katika hali mbaya kutokana na fedha kidogo inazopewa Halmashauri ya Serengeti ili kuitengeneza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiweka barabara hii katika uangalizi wa *TANROADS* ili iweze kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya matengezo ya uhakika ili kuondoa kero ya usafiri toka Mugumu hadi Arusha?

(b) Je, Serikali itakabidhi lini barabara hii kwa *TANROADS* na imetengewa kiasi gani cha fedha kwa ajili ya matengenezo ya uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu inaandaa *Road Act* itakayobadili sheria ya barabara ya mwaka 1969 *(The Highway Ordinance Cap. 167).* Tayari rasimu ya *Act* hiyo imekwisha kamilika na hivi sasa inapaitiwa na wadau kwa ajili ya kupata maoni ili iboreshwe.

Hivyo basi, zoezi la kupanga madaraja ya barabara nchi nzima linasubiri kukamilika kwa *Road Act* ambayo itatoa vigezo ambavyo vitawezesha kila barabara kuwa katika kundi ama daraja linalostahili. Iwapo barabara husika itakidhi kuwa barabara ya Mkoa, basi itakuwa imepandishwa na kuwa moja za barabara zitakazohudumiwa na Wizara ya Ujenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa vile barabara hii ya Mugumu - *Fort Ikoma* kwa sasa hivi ipo chini ya uangalizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, namwomba Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, awasiliane na Halmashauri ya Wilaya husika kujua

ni kiasi gani cha fedha zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya uhakika katika barabara hiyo.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuiarifu Wizara kwamba kazi nzuri imefanywa na *TANROAD* katika Wilaya yangu, lakini tatizo ni kwamba mpaka sasa miaka mitano inaisha hakuna Waziri ambaye amewahi kuja huku kuangalia mambo ya barabara, tunaomba Wizara hiyo imtume Waziri aje kule aangalie hali yetu ni mbaya.

**SPIKA:** Uliza swali basi.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Swali ni kwamba, je, ni lini watatembelea huko aidha, Waziri au Naibu Waziri kuja kuangalia? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sawa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi ni lini utatembelea huko?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tutajitahidi kupanga tuone tutafika huko lini, lakini tutajitahidi kupanga, sitaki kuahidi lini haswa lakini tutajitahidi kufika.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kwa sababu barabara hii sasa ni kiungo muhimu kati ya usafiri wa abiria toka Musoma kwenda Arusha na kwa kuwa sasa hivi wananchi wetu wengi wanatumia njia ya Kenya na barabara hii inaweza kuondoa tatizo la usafiri wa kupitia Kenya.

Je, Waziri anasemaje uwezekano wa Serikali kutoa fedha kuitengeneza barabara hii wakati tukisubiri hayo mabadiliko ya sheria aliyoitaja ?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, kama ifuatavyo:-

Najua barabara hii ni muhimu sana kutoka Musoma kwenda Arusha na vilevile najua kwamba Mkoa umeomba barabara hii iwe ya Mkoa, lakini kama nilivyosema mwanzoni ni kwamba tungoje sheria inayokuja ya barabara tuone kama itaipandisha hadhi hii barabara na juu ya kutoa fedha sasa hivi kutengeneza barabara hiyo, kwa kusema kweli hali ya Wizara ya Ujenzi iko kiasi kwamba hatuwezi ku-*reallocate* fedha kutoka barabara moja kwenda kwingine.

Mheshimiwa Spika, zile zilizokwishapangwa zimepangwa na tunajitahidi kuzitumia hivyo ili tuendane na Bajeti kama ilivyopangwa, nasikitika sana sasa hivi uwezo wa *reallocate* fedha Wizara ya Ujenzi hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bakari Mbonde, amemwachia swali lake Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, amuulizie, endelea Mheshimiwa Gama.

Na. 43

**Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Kati ya Kimanzichana - Kibiti.**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA (k.n.y. MHE. BAKARI M. MBONDE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkataba wa ujenzi wa barabara kati ya Kimanzichana Wilayani Mkuranga na Kibiti Wilayani Rufiji ulisainiwa baina ya Serikali na Mkandarasi tarehe 26 Mei, 2003 lakini hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2003 hakuna ujenzi wowote uliofanywa:-

(a) Je, kulikuwa na haja gani kwa Serikali kusaini mkataba wa ujenzi wakati ikifahamu kuwa utekelezaji wake usingeanza mapema?

(b) Je, ni sababu gani zilizofanya ujenzi wa barabara hiyo usianze kwa zaidi ya miezi saba baada ya kusaini mkataba?

(c) Je, Serikali inawapa matumaini gani wananchi wa Mkuranga na Rufiji kuhusu ujenzi wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mkataba kati ya Mhandisi Msimamizi, Kampuni ya *Gauff Engeneers* kutoka Ujerumani ulisainiwa tarehe 26 Mei, 2003 ili kusimamia kikosi cha ujenzi cha *TANROADS.* Mkataba huu ulikuwa na muda wa mwezi mmoja wa maandalizi, hivyo kazi zilipaswa kuanza mwanzoni mwa mwezi Julai, 2003 sambamba na kuanza kutolewa fedha za ndani na za nje kutoka mkopo wa Mfuko wa Kuwait. Hivyo kusainiwa kwa mkataba kulikuwa sahihi na haikutegemewa kuwa kazi zingechelewa kama ilivyotokea.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi zilichelewa sana kuanza hadi mwezi Desemba, 2003 kutokana na sababu kuu zifuatazo:-

(i) Kuchelewa kutolewa fedha za ndani.

(ii) Mhandisi kucheleweshа kufanya maandalizi ya awali yanayohusu, pia uandaaji wa nyaraka za zabuni za ununuzi wa vifaa vya ujenzi.

(iii) Mfuko wa Kuwait kuchelewa kutekeleza maombi ya mradi kulipia wazabuni.

(c) Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kurekebisha kasoro mbili za mwanzo zilizotajwa awali, Mfuko wa Kuwait umekuwa na ucheleweshaji usiokubalika wa kutowalipa wazabuni kama ilivyokubaliwa chini ya mkopo husika pamoja na kukumbushwa mara kwa mara na Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi. Hali hii imefanya mradi uliotegemewa kukamilika mwezi Februari, 2005 uzidi kuchelewa zaidi kwani kati ya kilometa 58 zilizotegemewa kukarabatiwa ni kilometa 13 tu ambazo zimeweza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha zinafanya jitihada na mawasiliano ya mwisho na mfuko wa Kuwait kabla haijaamua hatua za kuchukua kuzuia hasara inayozidi kuukabili mradi na kuamua njia nyingine za kukamilisha mradi huu.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Ni imani yangu wakati mnasaini Mkataba huu mlikuwa na muda maalum, je, kwa kuchelewa kwa sababu zilizotolewa Tanzania haiwezi ikashtakiwa na mwisho tukalipa gharama zaidi na mkandarasi husika?

(ii) Baada ya pesa hizo kutolewa na *Kuwait Fund* mnategemea barabara hii kutoka Kimanzichana hadi Kibiti itamalizika lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa mradi ukichelewa una gharama nyingi na mojawapo ni mkandarasi kudai, kwa hiyo, ndiyo maana tumesema katika jibu letu la mwisho kwamba tunawasiliana kwa mara ya mwisho na *Kuwait Fund* kama hawataweza basi tuweze kuweka utaratibu mpya kupunguza gharama hizo, gharama hizo ni pamoja na gharama za mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, kama fedha zikitolewa mradi huo unategemewa kumalizika lini, kwa sababu hatujui zitatolewa lini kwa hiyo ni vigumu kukadiria utamalizika lini, pesa zitakapopatikana ndipo hapo tutafanya *review* ya barabara hiyo na kutoa taarifa kwamba mradi utategemewa kumaliza lini.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi, pamoja na majibu mazuri na Naibu Waziri, tuna tatizo la mabaki ya lami ambayo

yanasababisha ajali kila siku kuanzia Bungu mpaka Kibiti. Je, lini atamwambia Mhandisi achonge hiyo barabara ili tusizidi kupata hasara ya matairi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Omar Chubi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijamwelekeza Mkandarasi kuchonga hiyo barabara kuondoa mabaki ya lami yanayoharibu matairi, naomba nipate muda mimi mwenyewe nikapite nione ni kiasi gani hasara hizo ili kuweza kuthibitisha, baadaye ndiyo nitoe maelekozo. Kwa sababu nikiahidi hapa kwamba nitatoa maelekezo na kumbe vipande vyenyewe vya lami si vibaya sana nitakuwa nimetia hasara mbili, kutoa taarifa ya uongo na kuelekeza vibaya. *(Kicheko)*

Na. 44

**Viwanda Vilivyoanzishwa Chini ya *TIC* kuhamia *EPZ***

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa *EPZ* ilianzishwa kuwawezesha wawekezaji wapya wa ndani na nje kuzalisha bidhaa kwa soko la nje; na kwa kuwa upo ujanja wa baadhi wa wawekezaji ambao wanakaribia kumaliza kipindi cha *tax holiday* kwa viwanda vilivyoanzishwa kwa kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* na sasa wanataka kuhamia *EPZ* ili waendelee na *tax holiday.*

(a) Je, Serikali inalifahamu jambo hilo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Serikali ina taarifa kuwa wapo wawekezaji waliowekeza kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC),* ambao wamemaliza na ambao hawajamaliza kipindi cha msamaha wa kodi *(tax holiday)* lakini wangependa kujiunga na programu ya *EPZ* kwa lengo la kupata vivutio vinavyotolewa chini ya mpango wa *EPZ.* Kwa rekodi zilizotolewa na *NDC* ambao ni wakala wa Serikali katika utekelezaji wa mpango wa *EPZ,* Makampuni saba yamewahi kuwasilisha maombi ya aina hiyo. Makampuni hayo ni *East Usambara Tea Company, OLAM (T) Ltd, Sunflag Arusha, Morogoro Canvas Mill, Seven Steel Mills Ltd, Premier Cashew Industries Ltd.* na *ISPO Industries Ltd.*

Hata hivyo, madhumuni ya kuanzisha mpango wa *EPZ* yalilenga zaidi katika kuanzisha viwanda kwa ajili ya mauzo ya nje *(export led industrialization)* kwa kuvutia

mitaji mipya, kuzalisha mazao mapya na kuanzisha masoko mapya. Kwa misingi hii, Baraza la *EPZ* lililoundwa kwa mujibu wa sheria ya *EPZ* lilitoa agizo linalosisitiza utoaji wa leseni za *EPZ* kulenga kwa wawekezaji wenye mitaji mipya tu. Kwa kuzingatia agizo hilo, hakuna mwekezaji ambaye alikwishapata vivutio chini ya sheria ya uwekezaji *(TIC)* na baadaye akapewa leseni *EPZ,* isipokuwa kiwanda cha URAFIKI ambacho kilipewa leseni ya *EPZ* kutokana na makubaliano maalum kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China.

(b) Hatua zinazochukuliwa na Serikali zinalenga katika kuhakikisha kwamba malengo ya kuanzisha mpango wa *EPZ* yanatekelezwa kwa misingi ya kanuni na taratibu zilizowekwa. *NDC* ambao ni wakala wa Serikali katika mpango wa *EPZ,* wanafanya juhudi kubwa kuwaelimisha na kuwaelewesha wawekezaji juu ya masharti ya kujiunga na mpango wa *EPZ.* Pia, Serikali ina mpango wa kuifanyia marekebisho sheria ya *EPZ* ili pamoja na mambo mengine, masharti ya kujiunga na mpango wa *EPZ* yawekwe bayana.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Ni lini sheria hiyo italetwa Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, kama ifuatavyo:-

Sheria hiyo italetwa Bungeni wakati muafaka na itakapokuwa tayari. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali unakaribia kuisha. Sasa matangazo ya vikao.

Lakini kwa utaratibu niliouweka jana wa kutambulisha wageni wa Waheshimiwa Wabunge wanaokuja hapa Bungeni kusikiliza shughuli zetu wanaomjulisha mapema Spika, leo napenda kuwatambulisha wageni wawili wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ambao wamekaa kwenye *gallery* upande wangu wa kulia na naomba wasimame ili tuwatambue. *(Makofi)*

*(Hapa wageni waliotambulishwa walisimama na kusalimia)*

**SPIKA:** Matangazo ya vikao vya leo, Kamati mbili zimepangiwa kukutana, Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anaomba wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 4.30 asubuhi hii mara baada ya maswali, anasema kwa muda mfupi tu. Chumba namba 107, ghorofa ya kwanza. Kamati ya Kilimo na Ardhi.

Kamati ya pili ni Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anaomba wajumbe wakutane asubuhi hii Ukumbi namba 231, ili kupitia taarifa ambayo itawasilishwa Bungeni. Kamati ya Miundombinu saa 5.00 asubuhi hii.

Mbali na Kamati, kuna *NGO* ya *Amani Forum* ya Wabunge, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wakutane leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi namba 133, ghorofa ya kwanza. Mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Kujiandaa, Kushirikiana na Kukabiliana na Janga la Kuvuja kwa Mafuta kutoka Melini na Kuharibu Mazingira wa mwaka 1990 *(International Convention on the Oil Pollution Preparedness, Response and Cooperation 1990)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha tamko la kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Kujiandaa, Kushirikiana na Kukabiliana na Janga la Kuvuja kwa Mafuta kutoka Melini na Uharibifu wa Mazingira *(International Convention of the Oil Pollution Preparedness Response and Cooperation 1990).*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa linalosimamia usafiri wa meli duniani yaani *International Maritime Organisation.* Shirika hili lina jukumu la kusimamia usalama wa usafiri wa majini pamoja na mazingira ya maji.

Ili kutekeleza jukumu hili Shirika limeandaa mkataba wa Kimataifa unaohusu kujianda kushirikiana na kukabiliana na janga la kuvuja kwa mafuta kutoka melini na kuharibu mazingira wa mwaka 1990. Ili kuwa na taratibu za kukabiliana na janga la kuvuja kwa mafuta kutoka kwenye meli.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu uliandaliwa kutokana na kuzidi kwa athari za matukio ya uchafuzi wa mazingira baharini kutokana na kuvuja mafuta kwenye meli, Kamati ya kulinda mazingira ya bahari ya Shirika la Kimataifa la usafiri wa majini ilianda mkataba huu ili kutoa mwongozo na ushirikiano wa Kimataifa katika *operation* ya kukabiliana na matukio makubwa ya uchavuzi wa mazingira kutokana na kuvuja kwa mafuta.

Mheshimwa Spika, maeneo muhimu ya kuzingatiwa katika mkataba huu ni yale yanayohimiza yafuatayo:-

(i) Wajibu wa mwenye meli iliyomwaga mafuta baharini atawajibika kulipa fidia.

(ii) Nchi mwanachama kuweka mikakati bayana ya hatua za kuchukua endapo ajali itatokea na umwagaji wa mafuta baharini.

(iii) Meli zilizosajiliwa na nchi mwanachama wa mkataba huu kuhakikisha zinabandikwa ndani ya meli ili hatua za haraka zinazotakiwa kuchukuliwa endapo kutatokea ajali ya umwagaji wa mafuta.

(iv) Ni wajibu wa meli kutoa taarifa za tukio la kumwagika kwa mafuta baharini na kutoa hatua za kufuata katika kupokea taarifa kama hiyo.

(v) Ni utaratibu wa Kitaifa kwa nchi jirani wa kusaidiana endapo ajali itatokea.

(vi) Ni wajibu wa nchi wanachama kutayarisha mikakati ya kufanya mafunzo kwa ajili ya kujiandaa namna ya kuzuia uchafuzi unaosababishwa na mafuta.

Mheshimiwa Spika, faida ya Tanzania kujiunga na Mkataba huu. Kwa kuwa Tanzania ni nchi yenye mwambao mrefu unaopitiwa na Meli za Kimataifa zinazobeba mafuta na pia uagiza maji kwa matumizi yake na matumizi ya nchi jirani kupitia bandari yake, upo uwezekano wa ajali kama hizi kutokea. Kwa kuridhia Mkataba huu kutakuwa na faida zifuatazo:-

1. Kulinda mazingira ya bahari yetu;

2. Kupata misaada na ushauri wa kitaalamu;

3. Kupata ushirikiano wa Kimataifa katika suala nzima la kukabiliana na kuvuja kwa mafuta kutoka kwenye meli;

4. Ni kuwa mwongozo wa kisheria wa namna ya kukabiliana na meli zinazohusika na usafirishaji wa mafuta;

Mheshimiwa Spika, pendekezo kwa kuwa faida ya kukubali na kuridhia Mkataba huu ni kubwa inapendekezwa kuwa Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likubali na kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu kujiandaa, kushirikiana na kukabiliana na janga la kuvuja kwa mafuta kutoka melini na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisome Azimio lenyewe.

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Kujiandaa, Kushirikiana na kukabiliana na Janga la Kuvuja kwa Mafuta Kutoka Melini na kuharibu mazingira *(The International Convention on the Oil Pollution Preparedness, Response and Cooperation, 1990).*

KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa unaohusu Kujiandaa, Kushirikiana na Kukabiliana na Janga la Kuvuja kwa Mafuta Kutoka Melini na Kuharibu Mazingira wa mwaka 1990 uliandaliwa kutokana na kuzidi kwa athari za matukio ya uchafuzi wa mazingira ya bahari kutokana na kuvuja mafuta kutoka kwenye meli:

NA KWA KUWA Mkataba unatoa maelekezo ya namna ya kushughulika uchafuzi wa mazingira ya bahari kunakosababishwa na umwagaji mafuta baharini:

NA KWA KUWA Tanzania ni nchi yenye mwambao mrefu unaopitiwa na meli za Kimataifa zinazobeba mafuta na pia huagiza mafuta kwa matumizi yake na matumizi ya nchi jirani kupitia bandari yake, upo uwezekano wa ajali kama hizi kutokea:

NA KWA KUWA Kamati ya Kulinda Mazingira ya Bahari ya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini iliandaa Mkataba huu ili kutoa mwongozo wa ushirikiano Kimataifa katika operesheni ya kukabiliana na matukio makubwa ya mchafuko ya bahari yanayosababishwa na mafuta:

NA KWA KUWA faida ya kuridhia Mkataba huu ni pamoja na:-

(a) Wenye meli kulazimika kuchukua tahadhari za kuzuia majanga kutokea kwenye eneo la ukanda wa bahari ya nchi yetu na hivyo kulinda mazingira ya baharini;

(b) Kupata misaada ambayo itasaidia kiteknolojia na kiujuzi katika kazi ya kudhibiti na kukabiliana na kuvuja kwa mafuta baharini;

(c) Kutakuwa na ushirikiano wa Kimataifa katika suala nzima la kukabiliana na kuvuja kwa mafuta kutoka kwenye meli;

(d) Kuwa na Mwongozo wa kisheria wa namna ya kukabiliana na meli zinazoshuka na usafirishaji wa mafuta;

(e) Kupata ushauri toka Mashirika ya Kimataifa yanayotafiti taratibu bora za namna ya kujiandaa na matukio ya umwagaji wa mafuta baharini;

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Saba na kwa Mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kwamba linaridhia.

Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Kujiandaa, Kushirikiana na Kukabiliana na Janga la Kuvuja kwa Mafuta kutoka Melini na Kuharibu Mazingira *(International on the Oil Pollution Preparedness, Response na Co-operation, 1990).*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ilikuwa na Maazimio sita ya kuwasilisha hapa na yote sita niliyapeleka kwenye Kamati inayohusika. Matano yalishughulikiwa jana na Mwenyekiti wa Kamati akatoa maoni kwa Maazimio yote sita. Kwa hiyo, hili limeshatolewa maoni ya Kamati sitamwita tena Mwenyekiti arudie aliyoyasema jana. Nitakwenda moja kwa moja kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Sasa sijapata ombi lolote la kuchangia Azimio hili. Kama yupo Mheshimiwa Mbunge anayetaka kuchangia bado orodha iko wazi. Lakini nilighafilika kumtambulisha wakati ule mgeni wa Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mbunge wa Nachingwea, naye yuko kwenye *gallery* ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Nachingwea Mheshimiwa Ali Athumani Kanga. Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kutoa maoni ya Kambi kwa Mujibu wa Kanuni ya Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c) na 81(1) Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haina matatizo ya kuridhiwa kwa Mkataba huu, ila tunaushauri na mambo tunayotaka Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi wake.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 22 cha Mkataba huu kinazungumzia juu ya lugha ambazo Mkataba huu umetafsiriwa kama vile, Kiingereza, Kichina, Kiarabu, Kifaransa, Kirusi na kadhalika, lakini Kiswahili hakimo kati ya lugha hizo, tunawashauri wale wakubwa wanaokwenda kutusainia mikataba wapige kelele ili Mikataba hiyo pia itafsiriwe kwa Kiswahili, kitu kitakachosaidia kukuza na kuendeleza lugha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 1 inayozitaka nchi mwanachama kujiandaa kukabiliana na janga la kuvuja kwa mafuta kutoka melini, Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni vipi Serikali imejiandaa kukabiliana na janga hilo wakati wanashughulikia kesi ya madai ya fidia toka kwa mwenye meli aliyesababisha uharibifu huo kama majanga yatatokea nchini petu.

Mheshimiwa Spika, suala la kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na mafuta baharini unahitaji kuwa na teknolojia ya kisasa, vifaa vya kisasa na madhubuti pamoja na wataalam waliobobea. Kambi ya Upinzani inamwomba Waziri atueleze, je Serikali imejiandaaje kwa mambo haya kabla ya kuridhia Mkataba huu? Kambi ya Upinzani inashauri kuwa ni vema Serikali ikajiandaa kukabiliana na janga hili kwa kuwa na vifaa, teknolojia na wataalam watakaokuwa tayari kudhibiti uchafuzi wa mazingira baharini haraka kabla ya kusambaa eneo kubwa la bahari yetu. Tuondokane na tabia ya kuridhia kila Mkataba unaokuja mbele yetu wakati utekelezaji wake ni mgumu kutokana na uchumi wetu kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani. Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie na pengine niongeze tu kwamba mimi nilikuwa mjumbe na nilikuwa Mwenyekiti wa kikao kilichojadili Mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri tulijadili umuhimu wa Tanzania kujiweka katika hali ya utayari yanapotokea majanga, na pia vilevile linapotokea tatizo kama hili ambalo linaloweza kutokana na meli kubwa ambazo zinatoka katika nchi kubwa. Tulifika mahali tukajadili na kuona kwamba si mafuta tu, lakini ufukwe wetu saa nyingine utatumika kwa kumwaga vitu vya hatari na kemikali za sumu. Nchi ambazo zina uwezo mkubwa zinafikia hatua kutumia bahari yetu kuu ambayo ni katika mpaka wetu wa zile kilomita 200 kumwaga uchafu au hata kemikali za hatari. Sasa tatizo kubwa ni kwamba uwezo wetu wa kuchunguza na kusimamia ufukwe huu ni mdogo.

Kwa hiyo, Kamati ilisisitiza sana na kuiomba Serikali kuchukua mfano wa Kenya. Wenzetu wa Kenya kwa umuhimu wa kuangalia suala la hali ya hewa na pia kuweka uwezekano wa kujua yanayotokea nchini waliombwa na Shirika la Hali ya Hewa la Kenya watoe rada, mara moja walitoa rada nne za kusaidia kutabiri na kusaidia kuona kwa umbali yanayotokea katika nchi. Sasa tumeomba na tumesisitiza sana kwamba Serikali ilichukulie hili na kulipa umuhimu kwa ajili ya kuitahadharisha nchi na kulinda haki ya nchi ni vizuri nchi izingatie kutoa vifaa vya kufanyia kazi katika utekelezaji wa Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona niliweka hili vizuri na nilisisitize sana kwamba ni vizuri tulitekeleze na tujiandae kwa kukabiliana na majanga. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, Kambi ya Upinzani tunashukuru na mengi kati ya hayo ni ushauri na Mheshimiwa Mbunge tunamhakikishia kwamba ushauri huo utachukuliwa na kama ameusoma Mkataba vizuri ni kwamba tutapata nafasi ya kupata taaluma mbalimbali zinazohusu maeneo haya kutoka Shirika la *IMO,* na kwa hiyo tunajiandaa kwa wataalam wetu kupata teknolojia hiyo ya kisasa. Vilevile niseme utekelezaji si ngumu kama kutakuwa na *determination once* tukipitisha hili ni lazima utekelezaji wake uende sambamba kwa sababu tumelikubali. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba ni kweli hiyo hatua tutaishughulikia na amesema tafsiri iwe kwa Kiswahili. Kwa sababu lugha nyingi zinazotumika hivi sasa na hivi karibuni AU walianza kutumia lugha ya Kiswahili. Nategemea labda katika Vyombo vya Kimataifa huko baadaye mambo yatabadilika na Kiswahili kinaweza kikatumika mpaka tutakapofikia hapo nadhani tafsiri ya mambo yetu ya *IMO* mengi yatakwenda kwa lugha ambayo tunaielewa na mtu wa kawaida anaweza kuisoma.

Pili, ni Mheshimiwa Henry Shekiffu tunamshukuru kwa mwongozo wake na maelekezo yake na ni kweli tulijadili kwa kina kama wewe ukiwa Mwenyekiti wakati ule, na ni kweli ulitoa maoni ya kwamba na sisi tujiandae angalau tupate hizo randa za kuona mbali. Mimi nasema hilo tunalichukua katika utekelezaji mzima wa suala hili na kama nilivyojibu Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba nchi inafaa sasa kujizatiti katika masuala haya. Ni vipi Serikali imejiandaa kukabiliana. Niseme Serikali imeandaa *contingency plan* ambayo kila bandari inayo kwa hivi sasa na *contingency plan* hii inatoa taratibu na mwongozo wa namna ya kutumia mafuta na kuendelea kuenea.

Mheshimiwa Spika, nasema mazoezi hufanywa kuhusu namna ya kujiandaa na tutaendelea kufanya hivyo kwa kutumia taratibu zetu tulizoziweka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu wengi tu wametoa ni mawazo na ushauri, nasema ushauri utazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Itifaki hii ipitishwe na Bunge lako Tukufu. Ahsanteni.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Kujiandaa,*
*Kushirikiana na Kukabiliana na Janga la Kuvuja kwa Mafuta*
*Kutoka Melini na Kuharibu Mazingira*
*liliridhiwa na Bunge).*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU NA JUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Maazimio ya Mikataba Mitano.

Kabla sijatoa maelezo ya awali, kuhusu Maazimio haya napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki na Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano wao ulioniwezesha kuboresha Maazimio haya.

Mheshimiwa Spika, Mikataba mitatu kati ya mitano inategemeana kwa kiasi kikubwa. Aidha, kutokana na mapungufu au mwanya wa Mkataba mmoja umesababisha Mkataba mwingine kupitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Mikataba hiyo ni:-

Kwanza, Azma ya Kutokomeza au Kutokuendeleza Utengenezaji na Matumizi ya Silaha za Nyuklia *(The Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty - NPT).*

Pili, Mkataba Unaokusudia Kutumia Nishati ya Nyuklia kwa Shughuli za Amani tu na sio katika Utengenezaji wa Silaha za Nyuklia *(Safeguards Agreements).*

Tatu, Itifaki ya Nyongeza *(Additional Protocol).*

Mikataba mingine miwili inahusu Jinsi ya kupashana Habari na Utoaji Misaada Pindi ajali ya kinyuklia inapotokea katika nchi ambayo ni Mwanachama. Mikataba hiyo ni:-

Nne, Misaada ya Kushughulikia Ajali ya Nyuklia au Dharura ya Kiradiolojia *(Convention on Assistance in the case of a Nuclear Accident or Radiological Emergency).*

Tano, Utoaji Taarifa Mapema juu ya Ajali ya Nyuklia *(Convention on Early Notification of a Nuclear Accident).*

Mikataba yote hii inasimamiwa na Shirika la Nguvu Atomiki Duniani *(the International Atomic Energy Agency - IAEA)* Hata hivyo, chanzo cha kupitisha Mikataba hii ni baada ya kutabiri kuwa ifikapo miaka ya 70 nchini nyingi duniani zingekuwa zinamiliki silaha za nyuklia. Hivyo, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa liliamua kuweka msimamo bayana ili kudhibiti utengenezaji na matumizi ya silaya za nyuklia ili kuepusha dunia na maangamizi yanayoweza kusababishwa na silaha hizo.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Azma ya Kutokomeza au Kutokuendeleza Utengenezaji wa Matumizi ya Silaha za Nyuklia *Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty - NPT* ni Mkataba uliopitishwa na Umoja wa Mataifa tarehe 12 Juni, 1968 kuhusu udhibiti wa matumizi, usambazaji na utengenezaji wa silaha za maangamizi ya binadamu unaotumia teknolojia ya nyuklia duniani. Hadi sasa Tanzania bado haijaridhia Mkataba wa *NPT* pamoja na Mikataba yake mingine ya kusimamia utekelezaji wake ambayo ni muhimu katika kuendeleza na kukuza matumizi salama na ya amani ya teknolojia ya nyuklia katika nyanja za elimu, afya, kilimo, utafiti, nishati, madini, maji, biashara na viwanda.

Vile vile Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakumbukwa imepitisha mwezi Aprili, 2003 Sheria ya Nishati ya Atomiki ili kuhamasisha na kuendeleza matumizi salama na ya amani ya teknolojia ya nyuklia kwa maendeleo ya Taifa. Teknolojia ya nyuklia inapatikana toka nje ya nchi kwa wahisani ambao hawawezi kutoa misaada inayohusika na teknolojia hii mpaka ithibitike kwamba nchi inayoomba msaada huo imeshasaini Mikataba inayohusika na usimamizi madhubuti wa nishati ya nyuklia na teknolojia zake, na hivyo teknolojia hiyo kuthibitishwa kuwa ni ya matumizi salama na ya amani.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu sasa nitapenda kutoa maelezo ya ziada ya jumla kuhusu kuridhia Mikataba Nishati ya Nyuklia na baadaye kuwasilisha nyaraka hizi katika mtiririko ufuatao:-

Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Azma Kutokomeza au Kutokuendeleza Utengenezaji na Matumizi ya Silaha za Nyuklia *Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty.* Misingi ya utekelezaji wa Mkataba huu wa *NPT* unaitaka kila nchi itakayousaini, kusaini pia Mkataba mwingine wa *Safeguard Agreements* kati yake na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani *(the International Atomic Energy Agency)* ambao ndiyo unaohusika na usimamizi wa utekelezaji wa *NPT.*

Mheshimiwa Spika, naomba kusoma Azimio lenyewe *NPT.*

Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Azma ya Kutokomeza au Kutokuendeleza Utengenezaji wa Matumizi ya Silaha za Nyuklia *(Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty.*

KWA KUWA Tanzania ni moja kati ya nchi zinazoendelea duniani na nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa,

KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa unaohusu Azma ya Kutokomeza au Kutokuendeleza Utengenezaji na Matumizi ya Silaha ya Nyuklia *(Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty)* ulipitishwa na Umoja wa Mataifa tarehe 12 Juni, mwaka 1968.

KWA KUWA hii ni kwa Mujibu wa Maazimio ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa yaliyotolewa kama ifuatavyo:-

(i) Azimio Na. 2346A la tarehe 19 Desemba, 1967;
(ii) Azimio Na. 2153A la tarehe 17 Novemba, 1966;

(iii) Azimio Na. 2149 la tarehe 4 Novemba, 1966;

(iv) Azimio Na.2028 la tarehe 19 Novemba, 1965;

(v) Azimio Na. 1665 la tarehe 4 Desamba, 1961

KWA KUWA Mkataba huu ulianza kutumika *(Entry into force)* mnamo mwezi Machi, 1970 baada ya nchi zilizoteuliwa kama nchi wahifadhi *(Depository Government)* kutoa matamko ya kuridhia *(Ratification instrument),* na nchi nyingine 40 kutia saini Mkataba huo kama ilivyoelezwa kwenye Ibara IX ya Mkataba.

KWA KUWA kupitishwa kwa Mkataba huo ni mojawapo ya juhudi za Kimataifa katika kutambua umuhimu wa kutokomeza utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia. Pia kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa katika matumizi salama na ya amani ya nishati nyuklia. Tangu Mkataba huo upitishwe jumla ya nchi 187 tayari zimekwisha saini Mkataba huo. Kati ya hizo, nchi 53 ni za Kiafrika. Mifano ya baadhi ya nchi za Kiafrika zilizokwisharidhia Mkataba huo ni:- Uganda, Kenya, Angola, Congo, Botswana, Msumbiji na Burundi.

KWA KUWA Tanzania ilisaini Mkataba huo mwaka 1991 lakini bado haijaridhia.

KWA KUWA Katika miaka ya 1960 ilitabiriwa kuwa nchi nyingi duniani (Kati ya 25-35) zitakuwa zinamiliki silaha za nyuklia ifikapo miaka ya 1970. Katika kukabiliana na hali hii majadiliano kuhusu Mkataba wa *NPT* yalianza.

KWA KUWA ilipofika mwaka 1968 Mkataba wa *NPT* ulipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa . Mkataba huo uliweka msimamo bayana dhidi ya utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia ili kuiepusha dunia na maangamizi yanayoweza kusababishwa na silaha hizo.

KWA KUWA Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa na vilevile ni mwanachma wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani *(The International Atomic Energy Agancy - IAEA)* inao wajibu wa kuridhia Mkataba huu ili kuungana na nchi nyingine duniani katika kupiga vita utengenezaji wa silaha za nyuklia.

KWA KUWA Kuridhia Mkatba huu kutaimarisha mfumo na mtandao wa kudhibiti silaha za nyuklia duniani kote. Pia Tanzania itanufaika na misaada inayohusu teknolojia ya nyuklia kwa maendeleo ya nchi.

KWA KUWA Ibara ya I ya Mkataba huu inazitaka nchi zilizotia saini Mkataba huo na pia zenye silaha za nyuklia kutokuruhusu kuhamisha silaha hizo kwenda nchi nyingine kwa namna moja au nyingine. Pia kutoshawishi au kutosaidia nchi zisizo na silaha za nyuklia kutengeneza au kupata silaha hizo.

KWA KUWA Ibara ya II ya Mkataba huu inazitaka nchi zisizomiliki silaha za Nyuklia kutokupokea silaha hizo au vifaa vingine vinavyohusika na utengenezaji wa silaha za nyuklia. Pia kutopokea msaada unaohusu utengenezaji wa silaha hizo kutoka nchi nyingine.

KWA KUWA Ibara III ya Mkataba inahusu wajibu wa nchi zilizotia saini Mkataba huo kusaini Mkataba wa *Safeguards* kati yake na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani kulingana na Katiba iliyounda Shirika hilo.

KWA KUWA Tanzania itanufaika na misaada inayohusu teknolojia ya nyuklia kwa maendeleo na ustawi wa wananchi wake. Vinginevyo Jumuiya ya Kimataifa haipo tayari kuisaidia nchi yetu katika kuendeleza teknolojia hii ya nyuklia kwa maendeleo ya Taifa. Pia Tanzania itakuwa na nafasi nzuri ya kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kudhibiti utengenezaji wa silaha za nyuklia na matumizi yake.

KWA KUWA hakuna mahitaji yoyote ya fedha zaidi ya michango ya kawaida ya Tanzania katika Baraza la Umoja wa Mataifa.

KWA HIYO BASI baada ya kuona umuhimu wa kuridhia Mkataba huu Serikali ya Tanzania ikubali kuridhia Mkataba na Bunge lako Tukufu kuridhia wa Kimataifa unaohusu Azma ya Kutokomeza au Kutokuendeleza Utengenezaji na Matumizi ya Silaha za Nyuklia *(Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty. NPT)*

Nawasilisha Azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, *Safeguards Agreement* ni Mkataba wa Kimataifa unaokusudiwa kutumia nishati ya nyuklia kwa shughuli za amani tu na siyo katika utengenezaji wa silaha za nyuklia. Mkataba huu wa *Safeguards Agreement* ulitayarishwa baada ya kugundulika kwamba baadhi ya nchi ambazo tayari zilikwishasaini Mkataba wa *NPT* kuthibitika kujihusisha na majaribio ya utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia kinyume na Mkataba wa *NPT.*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kusoma Azimio lenyewe la *Safeguards Agreement.*

KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa unaohusu Kukomesha Silaha za Nyuklia *(Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty NPT)* unazitaka nchi zote ambazo hazina silaha za nyuklia na ambazo zimetia saini Mkataba huo kutia saini Mkataba mwingine uitwao *the Safeguards Agreement.*

Yaani Mkataba unaokusudia kuhakikisha kuwa nishati ya nyuklia inatumiwa katika shughuli ambazo ni za amani tu na sio katika utengenezaji wa silaha. Nchi hizo zitatia saini Mkataba huo kati yake na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani *(the International Atomic Energy Agency)* kama ilivyoelezwa katika Ibara III ya *NPT* na Katiba ya *IAEA.*

KWA KUWA IAEA imepewa wajibu wa kuhakikisha kuhakikisha kuwa nyenzo au shughuli yoyote ya kinyuklia inayofanyika kwa msingi wa amani haibadilishwi na kutumika kutengeneza silaha au milipuko yoyote ya kinyuklia.

NA KWA KUWA Tanzania kama nchi iliyotia saini *NPT* na vile vile kama nchi mwanachama wa *IAEA* ilitia saini *Safeguards Agreement* mnamo tarehe 27 Agosti, 1992, lakini Mkataba huo haujaanza kutumika wala kuridhiwa. Nchi nyingi zikiwemo za Afrika pia zimetia saini hata kuridhia Mkataba huo. Kwa mfano, Angola, Kenya, Uganda na Botswana.

KWA KUWA Tanzania inatumia nishati ya nyuklia kwa matumizi salama na ya amani ya uchumi na ya maendeleo yakiwemo katika hivyo viwanda, kilimo, tiba, utafiti na elimu. Kwa vile Tanzania haitegemei kutumia nishati ya nyuklia tofauti na maeneo yaliyotajwa hapo juu yaani katika utengenezaji wa silaha za nyuklia.

NA KWA KUWA Serikali inatakiwa ikubali kuridhia Mkataba huu ili kujijengea imani kwa Jumuiya ya Kimataifa na hivyo kunufaika zaidi na misaada ya teknolojia ya nyuklia kutoka *IAEA* na Taasisi nyingine ya Kimataifa katika shughuli mbalimbali kama zilivyotajwa hapo juu.

Kwa mfano, hivi karibuni Tanzania imenufaika na msaada wa teknolojia hiyo katika kutokomeza Mbung'o huko Zanzibar na Visima vya Mafia. Msimamo wa Kimataifa sasa hivi misaada ya aina hiyo haiwezi kutolewa kwa nchi ambazo hazijaridhia Mkataba kama huu.

KWA KUWA Ibara ya II ya Mkataba inatoa wajibu kwa *IAEA* kuhakikisha kuwa katika nchi husika shughuli zote zinazohusika na nishati ya nyuklia zinatumika kwa matumizi ya amani na siyo vinginevyo.

KWA KUWA Ibara ya IV ya Mkataba inafafanua kuwa utekelezaji wa Mkataba huu hautaingilia shughuli za amani za nishati ya nyuklia zinazofanyika nchini isipokuwa pale zinapotumika tofauti na matumizi ya amani kama ilivyoainishwa katika kiambatanisho nne wakati wa kutia saini Mkataba huu.

KWA KUWA Ibara ya VII ya Mkataba inataka Tanzania kuweka Mfumo utakaohakikisha udhibiti wa shughuli zote zinazotumia nishati ya nyuklia kulingana na matakwa ya Mkataba huo.

KWA KUWA Ibara ya VIII ya Mkataba huu inahusu wajibu Watanzania kutoa taarifa kwa *IAEA* kuhusiana na shughuli ilizonazo za kinyuklia ambazo zitahusika Mkataba huu.

KWA KUWA Ibara ya IX ya Mkataba huu inahusu *IAEA* kuteua wakaguzi baada ya kupata kibali kutoka Serikali ya Tanzania kwa ajili ya shughuli za ukaguzi nchini.

KWA KUWA hakuna mahitaji yoyote ya fedha isipokuwa zile za uendeshaji wa Mkataba huu zilivyoelezwa katika Ibara ya 15.

KWA KUWA Mkataba huu utaiwezesha Tanzania kunufaika na misaada inayohusu teknolojia ya nyuklia kwa matumizi salama na ya amani.

HIVYO BASI Baada ya kuona umuhimu wa kuridhia Mkataba huu na kuzingatia kwamba Tanzania kama itasaini Mkataba huu itanufaika na misaada itakayotolewa na Jumuiya ya Kimataifa katika kuendeleza matumizi salama na ya amani ya teknolojia ya nyuklia na maendeleo ya Taifa na siyo katika utengenezaji wa silaha za nyuklia yaani *Safeguards Agreement*. Sasa Bunge lako Tukufu linaombwa kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusaini *Safeguards Agreement* bado baadhi ya nchi zimekuwa haziainishi baadhi ya nyuklia materials walizonazo.

Kwa msingi huo Itifaki ya nyongeza yaani *Additional Protocol* ya Mkataba wa Kimataifa ya usimamizi madhubuti wa *Safeguards Agreement* ilipitishwa hapa mwaka 1997.

Lengo la Itifaki hii ni kuweka mfumo madhubuti wa kupata taarifa zaidi kuhusu mipango iliyopo na ya baadaye ya shughuli za kinyuklia ili kuwa na uwezo zaidi wa kusimamia na kukagua shughuli zote za kinyuklia zilizoainishwa na zile zisizoainishwa yaani *declared and undeclared nuclear materials* kutoka katika nchi husika.

Utekelezaji wa itifaki hii unatoa kibali au unaruhusu wakaguzi wa Kimataifa silaha za nyuklia kuhusika na maeneo ambayo hayakuainishwa yaani *undeclared nuclear materials* katika mikataba ya *NPP* na *Safeguards Agreement* na hivyo kutokutoa mwanya kwa nchi nyingine kuendeleza majaribio ya silaha za nyuklia.

Mheshimiwa Spika, naomba ruhusa ya kusoma Azimio lenyewe *Additional Protocol.* Azimio la kuridhia itifaki *Additional Protocol* ya Kimataifa ya usimamizi madhubuti wa *Safeguards Agreement.* Kwa kuwa itifaki ya Kimataifa *Additional Protocol to SafeGuards Agreements* imeidhinishwa na bodi ya magavana ya shirika la nguvu za atomiki duniani *(International Atomic Energy Agency)* mwezi Mei mwaka 1997. Itifaki hii inaipa *IAEA* mamlaka zaidi ya kupata habari zinazohusiana na *program* za nyuklia za nchi mbalimbali zilizo saini *Safeguards Agreements* yaani mikataba inayokusudia kutumia nishati ya nyuklia kwa shughuli za amani tu na siyo katika utengenezaji wa silaha za nyuklia.

Kwa kuwa lengo kubwa la itifaki hii ni kuwepo mfumo madhubuti wa kusimamia na kukagua shughuli zote za nyuklia zilizo ainishwa na zile zisizo ainishwa *declared and undeclared nuclear materials activities.* Ili kuhakikisha kwamba hazitumiki kwa madhumuni ya kutengeneza silaha za nyuklia kwa kuwa hatua hii imechukuliwa baada ya nchi kadhaa zilizo saini *Safeguards Agreements* kuonyesha udanganyifu au kutumia nyenzo za nyuklia kutengeneza silaha za nyuklia badala ya matumizi ya amani kama takiwa na *Safeguards Agreements* hivyo kutishia amani ya dunia. Kwa kuwa nchi nyingi duniani zimesha saini itifaki hii zikiwemo nchi za kiafrika ambazo ni pamoja na Ghana,

Mali, Namibia, Nigeria na Afrika Kusini. Tanzania bado haija saini wala kuridhia itifaki hii.

Kwa kuwa itifaki hii ni nyongeza ya Safeguards Agreements ambayo Tanzania imekwisha saini ni vema Tanzania ikasaini na kuridhia itifaki hii ili kuungana na jumuiya ya Kimataifa katika kuweka mfumo madhubuti wa kuhakikisha kwamba nishati ya nyuklia haitumiki katika utengenezaji wa silaha. Hivyo kuitaka Serikali iridhie itifaki hii ili kuiweka nchi katika nafasi nzuri ya kuendelea kupokea misaada inayohusu matumizi salama na ya amani ya teknolojia ya nyuklia kwa maendeleo ya nchi yetu. Hii ni pamoja na kushirikiana na nchi nyingine katika masuala ya utafiti na mafunzo yanayohusu teknolojia ya nyuklia.

Kwa kuwa itifaki hii itawezesha Tanzania kunufaika kwa misaada inayohusu teknolojia ya nyuklia kwa matumizi salama na ya amani katika nyanja mbalimbali za uchumi na maendeleo kama vile kuzalisha nguvu za umeme kwa kutumia nishati hii ya nyuklia vile vile itifaki hii itawezesha Tanzania kushirikiana na nchi nyingine katika masuala ya utafiti mafunzo yanayohusu teknolojia ya nyuklia.

Aidha umuhimu wa kusaini itifaki hii umetiwa msisitizo katika nakala ya barua iliyoambatanishwa kutoka kwa wafadhili wa umoja wa Mataifa. Kwa kuwa ulituridhia itifaki hii kutaliwezesha shirika la *IAEA* kupata taarifa zaidi kutoka katika nchi husika zinazohusu nyenzo au shughuli na mipango ya baadaye inaweza kuandaliwa ya matumizi ya nishati ya nyuklia yasiyokuwa ya amani, kingine ni yale yaliyokwisha ainishwa chini ya *A Comprehensive Sectors Agreements.* Pia kutawezesha wakaguzi kutoka shirika la nguvu za atomiki duniani *IAEA* kudhibiti mada zenye mionzi ya nyuklia au shughuli zinazotumika kwa zinazotumia mionzi ya nyuklia katika eneo lolote la nchi hazifanywi kwa malengo ya kutengeneza silaha za nyuklia.

Kwa kuwa nchi inayotaka kuridhia itifaki yaani *Protocol Additional to Safeguards Agreements* haina budi kufuata utaratibu iliyojiwekea kwa katiba ambapo Serikali kupitia Wizara husika inatakiwa ipeleke hoja Bungeni ili Bunge liweze kutoa tamko la kuridhia *Ratification Declaration* na hivyo kuufanya mkataba huu au itifaki hiyo kuwa sehemu ya sheria za nchi. Baada ya Bunge kutoa tamko la kuiweka kisheria *ratification istment* hatua zifuatazo zinapaswa kufuatwa.

Kwa kuwa nchi husika itapaswa kutoa taarifa *IAEA* kuhusu nia au kusudio la kukabiliana itifaki *Additional Protocol* pia kuwaomba *IAEA* kuwasirisha rasimu za kusudio hilo kwa bodi ya Magavana ili itoe idhini kwa Mkurugenzi Mkuu kutia saini, kwa kuwa hakuna mahitaji yote ya fedha zaidi ya gharama zitakazo husiana na uendeshaji katika kutekeleza itifaki hii kwa hiyo basi bunge la Serikali ya Tanzania linaombwa kukubali kuridhia itifaki *Additional Protocol* ya Kimataifa ya usimamizi madhubuti wa *Safeguard Agreements.* Ninawasilisha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuelezea mikataba miwili iliyobakia ambayo niliitaja hapo awali. Mikataba hii miwili inahusika zaidi na utekelezaji wa kila siku wa *NPT* umuhimu wa mikataba hii unajitokeza baada ya kutambua kwamba katika matumizi

ya amani ya teknolojia hii ajali yaweza kutokea hivyo ni muhimu kuwepo na mkataba utakao simamia utoaji misaada kwa nchi husika ambao ni mwanachama pindi ajali ya nyuklia itakapo tokea.

Pia mkataba mwingine umuhimu ulipitishwa kwa jinsi ya kupashana habari kuhusu ajali hizo za nyuklia. Mikataba hii inategemeana kwa kiasi kikubwa hivyo ni vyema yote tukairidhia kwa pamoja. Mikataba hiyo ni Misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura ya kiradiolojia *(The Assistance In The Case Of Nuclear Accident Or Radiological Emergency).* Mkataba huu unahusika na utoaji misaada za kushughulikia ajali za nyuklia au dharura za ki-radiolojia.Mkataba huu ni mmoja kati ya mikataba mingine iliyopitishwa chini ya *IAEA* kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa mkataba wa *NPT.* Mkataba mwingine unaofanana na huu unahusu utoaji taarifa mapema juu ya ajali za nyuklia *(Convention on Early Notification of a Nuclear Accident).*

Mheshimiwa Spika naomba ruhusa kusoma Azimio lenyewe la *The Assistance In Case Of A Nuclear Accident.* Azimio la kuridhia mkataba unaohusu misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura ya ki-radiolojia. Kwa kuwa mkataba unaohusu misaada kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura ya ki-radiolojia ulipitishwa na mkutano mkuu wa shirika la nguvu za atomiki duniani *(The International Atomic Energy Agency)* katika kikao chake maalum kilichofanyika tarehe 24/26 Septemba mwaka 1986 mjini Vienna, Austria. Kwa kuwa mkataba huu ulifunguliwa rasmi kwa ajili ya kutiwa sahihi na Mataifa mbalimbali tarehe 26 Septemba, 1986 huko Vienna, Austria na tarehe 6 Oktoba, 1986 huko New York, Marekani. Kwa kuwa kupitishwa kwa mkataba huu ni moja ya juhudi za Kimataifa za kuhakikisha usalama wa hali ya juu katika shughuli zote zinazohusu nishati ya nyuk lia na mkazo zaidi ni kuzuia uwezekano wa ajali kutokea au kupunguza kwa kiwango kikubwa madhara ya ajali hiyo endapo itatokea.

Ijapokuwa nchi nyingi tayari zimekwisha saini na kuridhia mkataba huu Tanzania bado haija saini wala kuridhia mkataba huu. Kwa kuwa mkataba unaohusu misaada ya kushughulikia ajali au dharura ya ki-radiolojia uliyopitishwa na shirika la nguvu za atomiki unagusa nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania zinazotumia nishati ya nyuklia katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, maendeleo na yale maeneo mengi ambayo ni pamoja na mahospitali, tiba na uchunguzi wa magonjwa, viwandani, kilimo, sekta ya elimu na kufundishia.

Kwa kuwa ni muhimu kuitaka Serikali bado kuridhia mkataba huu ili Tanzania iingie kwenye mfumo wa Kimataifa ambao utawezesha upatikanaji wa misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia endapo itatokea na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa madhara yake kwa kuwa Tanzania itanufaika na misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura ya ki-radiolojia endapo itatokea nchini au nchi nyingine jirani na hivyo kulinda maisha ya wananchi wake mali na mazingira. Pia Tanzania kama nchi mwanachama wa shirika la nguvu za atomiki duniani itaendelea kunufaika na misaada ya kiufundi toka shirika hilo katika shughuli za kushughulikia dharura za ki-nyuklia *either* kusaini mkataba huu Tanzania itaimarisha zaidi ushirikiano uliopo kati yake na Mataifa mengine duniani katika eneo hili.

Kwa kuwa Ibara ya 1 ya mkataba huu inazitaka nchi zitakazotia saini mkataba huu yaani nchi wanachama kushirikiana miongoni mwao na pia kushirikiana na shirika la nguvu za atomiki duniani ili kuwezesha upatikanaji wa msaada wa kushughulikia ajali au dharura ya ki-radiojia kwa madhumuni ya kupunguza madhara yake na hivyo kulinda maisha ya binadamu nayo mazingira.

Kwa kuwa Ibara ya 2 ya mkataba huu unahusu msaada wakati wa ajali ya nyuklia kwamba nchi inayohitaji msaada huo bila kujali kama ajali hiyo imetokea ndani ya nchi hiyo ama nchi nyingine itafanya hivyo kwa kuomba msaada huo toka nchi nyingine au kutoka shirika la nguvu za atomiki duniani. Nchi inayoomba msaada itaeleza aina ya msaada unaotakiwa na kama inao uwezo wa kutoa msaada unatakiwa pia endapo inaweza kuomba msaada unaohusu matibabu ama kazi ya muda katika nchi nyingine kwa watu walioathirika na ajali hiyo.

Kwa kuwa Ibara ya 7-inahusu gharama zitakazo husika na utoaji wa msaada wa kushughulikia au kudhibiti ajali ya nyuklia au dharura ya ki-radiolojia nchi inayotoa msaada inaweza kufanya hivyo bila kudai gharama yoyote kutoka kwa nchi inayosaidiwa na katika kufanya hivyo itazingatia yafuatayo: -

* Chanzo na aina ya ajali au dharura ya ki-radiolojia inayotokea.
* Mahali ajali au dharura ya ki-radiolojia ilipotokea.

* Mahitaji ya nchi ambazo hazina shughuli nyingi zinazohusu misaada ya nyuklia pamoja na mambo mengineyo.

Kwa kuwa endapo nchi inayotoa msaada itataka kurudishiwa gharama ilizotumia katika kutoa msaada huo basi inchi iliyopewa msaada huo italazimika kurudisha gharama hizo hata hivyo inchi yoyote wakati wa kuridhia mkataba huu inaweza kutamka kuwa haifungwi na kipengele cha kurudisha gharama za msaada iliyopewa. Kwa kuwa nchi inayotaka kuridhia mkataba unaohusu misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura za ki-radiolojia *(The Convention Assistance in Case Of Nuclear Accident On Radiological Emergency)* haina budi kufata utaratibu iliyojiwekea kikatiba.

Kwa kuwa hakuna mahitaji ya fedha katika kuridhia na kutekeleza mkataba huu isipokuwa gharama zinazohusiana na msaada wa kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura ya ki-radiolojia endapo nchi itaamua kufungwa na kipengele hicho kama ilivyoelezwa kwenye ibara ya 7 ya aya ya 2 na ya 3 ya mkataba. Kwa hiyo, basi kutokana na umuhimu wa kuridhia mkataba huu inapendekezwa kwamba bunge lako Tukufu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikubali kuridhia mkataba huu, unaohusu misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura za ki-radiolojia *(The Convention On Assistance In The Case Of Nuclear Accident Of Radiological Emergency).* Naomba kuwasilisha Azimio hilo.

Mheshimiwa Spika mwisho utoaji taarifa mapema juu ya ajali ya nyuklia *(Convention On The Early Notification Of Nuclear Accident).* Mkataba huu unafanana na ule wa *Radiological Emergency* ambao unasimamia utekelezaji wa mkataba wa *NPT.*

Mkataba huu ni muhimu sana maana unahusu upashanaji habari pindi ajali ya ki-nyuklia itakapojitokeza ndani au nje ya nchi. Kutokana na taarifa hizo kusambazwa kwa nchi wanachama nchi iliyopatwa na ajali itapata msaada wa haraka pasipo gharama zozote. Pia nchi nyingine baada ya kupata taarifa hizo zitapata fursa ya kutoa msaada wa haraka.

Mheshimiwa Spika naomba sasa kusoma Azimio lenyewe *(The Early Notification Of Nuclear Accident).* Kwa kuwa mkataba wa Kimataifa unaohusu utoaji taarifa mapema juu ya ajali yoyote ya nyuklia (*Convention On The Early Notification Of Nuclear Accident)* ulipitishwa na mkutano mkuu wa shirika la nguvu za atomiki duniani katika kikao chake maalumu kilichofanyika tarehe 24/26 Septemba, 1986 kufuatia ajali ya milipuko wa mitambo ya nyuklia *Chino Bill* huko Urusi.

Kwa kuwa mkataba huu ulisainiwa kwa mara ya kwanza na Mataifa yote mnamo tarehe 26 Septemba, 1986 huko Vienna, Austria na baadaye mkataba huu ulifunguliwa tena tarehe 6 Oktoba, 1986 huko New York, Marekani mkataba huu ulianza kutumika *Reality Entered Into Fourth* tarehe 27 Oktoba, 1986 siku 30 baada ya tawi la kwanza la kufunguliwa kwa ajili ya kutiwa saini ambapo nchi tatu zilitiasaini mkataba huo ambazo ni Denmark, Malaysia na Norway kama inavyotakiwa na Ibara ya 12 ya mkataba huo.

Kwa kuwa kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya nyuklia katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya binadamu duniani inabainika kwamba upo uwezekano wa kusababisha madhara makubwa kwa binadamu na mazingira yake katika nchi husika na zile zinazopakana endapo ajali itatokea mahala popote duniani hivyo mkataba huu utaiwezesha nchi inayohusika na ajali kutoa taarifa mapema za ajali hiyo na kupatiwa misaada ya haraka kutoka nchi nyingine katika kudhibiti madhara yanayoweza kutokea kutokana na ajali hiyo.

Teknolojia ya nyuklia hutumika sana katika mahospitali kwa mfano tiba, kuchunguza magonjwa, viwanda, elimu, kilimo, tafiti, vinu vya kuzalisha nguvu za umeme na kadhalika. Kwa kuwa kutokana na uwezekano mkubwa wa kutokea ajali ya nyuklia katika shughuli zilizotajwa hapo juu Jumuiya ya Kimataifa imeamua kuanzisha mfumo wa kupashana habari miongoni mwa wanachama endapo ajali ya nyuklia itatokea katika nchi yoyote ile duniani kutokana na uwezekano wa ajali kama hizo kuvuka mipaka au kusambaa hadi nchi jirani.

Hii itasaidia nchi husika kupata msaada wa haraka kutoka shirika hilo la atomiki la duniani na nchi nyingine duniani. Nchi nyingine zisizo husika moja kwa moja na ajali hiyo nazo zitapewa taarifa mapema iwezekanavyo ili kujiandaa kikamilifu kukabiliana na ajali hiyo na hata kuchukua hatua za tahadhari zinazotakiwa ikizingatiwa kwamba ajali yaweza kutokea katika nchi moja lakini madhara yake yakasambaa katika nchi nyingine za jirani.

Kwa kuwa mkataba huu ni moja ya hatua muhimu katika mfumo huo unaokusudia kuziwezesha nchi wanachama kupashana habari na taarifa za ajali ya nyuklia tangu mkataba huu kutiwa saini kwa mara ya kwanza nchi nyingi zikiwemo zinazoendelea zimesha saini na hata kuridhia mkataba huo. Kwa kuwa Tanzania bado

haija saini wala kuridhia mkataba huo hivyo ni muhimu kuitaka Serikali ya Tanzania na bunge lako Tukufu waungane na nchi nyingine duniani kwa kudhiria mkataba huu. Mifano ya nchi za Kiafrika zilizokwisha ridhia mkataba huu ni *Cameroon, Cote d'Ivoire, Egypt,* Tunisia, Sudan, Senegal, Mali, Nigeria, Afrika ya Kusini na Zimbabwe. Kwa kuwa Ibara ya 1 ya mkataba inaelezea shughuli ambazo zinahusika na ajali ya nyuklia shughuli hizo ni pamoja na kinu cha nyuklia kwa ajili ya kuzalisha umeme au tafiti ya *The Nuclear Reactor,* kinu cha kuzalisha mzunguko wa nishati ya nyukilia *(Nuclear Fuel Cyclic Facility),* vifaa vya takataka za mionzi *(Radioactive Waste Management Facility),* usafirishaji wa vyanzo vya mionzi na takataka zake, uzalishaji matumizi, uhifadhi, utupaji na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi kwa madhumuni ya kilimo, viwanda, mahospitali, elimu na utafiti.

Kwa kuwa Ibara ya 2 ya mkataba huo inahusu utoaji wa taarifa na habari za ajali ya nyuklia ambapo nchi inayotoa taarifa itafanya hivyo haraka iwezekanavyo. Taarifa hiyo inaweza kupelekwa moja kwa moja katika shirika la nguvu za atomiki duniani ila taarifa hiyo itapendekeza jinsi ya kupunguza kiwango cha madhara yatakayotokana na ajali hiyo. Kwa kuwa Ibara ya 3 ya mkataba inahusu utoaji wa taarifa za ajali au matukio hatari yanayotokana na shughuli zozote zile zinazohusu matumizi ya vyanzo vya mionzi ya nyuklia zinazoweza kujitokeza kutokana na shughuli nje ya zile ambazo zimetajwa yaani *Unpredicted Incidents.* Kwa kuwa Ibara ya 4 ya mkataba inaainisha majukumu ya shirika la atomiki duniani endapo ajali itakuwa imetokea shirika la atomiki la duniani litawajibika kuzifahamisha nchi nyingine zitakazo athirika na ajali hiyo na pia mashirika mengine ya Kimataifa baada ya shirika la Kimataifa la nguvu za atomiki kupokea taarifa hizo kutoka kwa nchi inayotoa taarifa.

Kwa kuwa Ibara ya 5 inaeleza mfumo na utaratibu wa kutoa taarifa ambapo taarifa inayotolewa inapaswa na takwimu zifuatazo:-

* Muda na mahali ajali ya nyuklia ilipotokea;
* Mtambo au chombo kilichohusika na ajali kinachosadikiwa kuwa ni chanzo cha ajali;
* Na uwezekano wa ajali kuendelea na hata madhara yake kuvuka mpaka;
* Tabia *(characteristics)* za uvujaji wa mionzi
* Mfumo wa kudhibiti mazingira kuhusiana na uvujaji wa mionzi kuvuka mpaka;
* Hatua zinazochukuliwa kudhibiti au kuzuia ajali hiyo.

Kwa kuwa hakuna mahitaji yoyote ya fedha zaidi ya gharama zitakazohusiana na utoaji wa taarifa endapo ajali itatokea Tanzania kwa hiyo basi kuridhia mkataba huu kutaiwezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupokea na kutoa taarifa za ajali ya nyuklia kwa nchi nyingine au kwa shirika la atomiki duniani mapema iwezekanavyo na hivyo kuwa na nafasi nzuri ya kupatiwa msaada katika kukabiliana na ajali kama hiyo endapo itatokea nchini vile vile nchi yetu kwa kupata taarifa zinazohusu ajali ya nyuklia zilizotokea katika nchi nyingine duniani itaweza kujiandaa kikamilifu katika kukabiliana na tatizo kamili hilo endapo litatokea nchini.

Mheshimiwa Spika napenda kuomba Bunge lako Tukufu kupokea Azimio hili na kuliridhia.

Mheshimiwa naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW'- MWENYEKITI KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika awali ya yote naomba nitoe shukrani kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii uliyoipa jukumu la kufikiria maazimio matano ya kuridhia mikataba ya Kimataifa ambayo inasimamiwa na shirika la nguvu za atomiki duniani *(The International Atomic Energy Agency)* ambalo Tanzania ni mwanachama tangu 1976.

Mheshimiwa Spika maazimio yanayoridhia mikataba hiyo ni matano na kutokana na ukweli kwamba mikataba hiyo inategemeana kwa kiasi kikubwa na maelezo iliyotolewa na Serikali kuwa upungufu katika mkataba mmoja ulisababisha kuandaliwa kwa mkataba mwingine kamati inatoa maoni yake kwa mikataba yote mitano kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika kamati yangu ilipata maelezo fasaha ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu, kuhusu umuhimu wa Azimio ya Bunge ya kuridhia mikataba ya Kimataifa ifuatayo:-

1. Mkataba wa Kimataifa unaohusu azma ya kutokomeza au kutoendeleza utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia *(Non-Proliferation of Nuclear Weapons Treaty) NPT.*

2. Mkataba wa Kimataifa unaokusudia kutumia nishati ya nyuklia kwa shughuli za amani tu na si katika utengenezaji wa silaha za nyuklia *(Safeguard Agreement)*

3. Itifaki ya nyongeza *(Additional Protocol)* ya mkataba wa Kimataifa ya usimamizi madhubuti wa *Safeguard Agreement*

4. Mkataba wa Kimataifa unaohusu utoaji wa taarifa mapema juu ya ajali ya nyuklia *(Convention On Early Notification Of A Nuclear Accident).*

5. Mkataba wa Kimataifa unaohusu misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura ya ki-radiolojia *(Convention on Assistance in Case of Nuclear Accident or a Radiological Emergency).*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi inayopenda amani, upendo, utulivu na mshikamano na kwamba Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na ilijiunga na shirika la nguvu za atomiki duniani mwaka 1976 na pia kuwa Bunge la Tanzania lilipitisha sheria ya matumizi ya nishati ya atomiki mwezi Aprili, 2003 kwa lengo la kuhamasisha na kuendeleza matumizi salama na ya amani ya teknolojia ya nyuklia.

Mheshimiwa Spika Kamati yangu inaunga mkono maazimio haya kwa kuzingatia kuwa nchi yetu imekuwa ikinufaika na misaada iliyowezesha kuingiza teknolojia inayotumia nishati ya nyuklia kwa ajili ya matumizi salama na ya amani kwa manufaa na maendeleo ya nchi katika matumizi. Kwa mfano, mashine za *X-ray,* tiba ya saratani, utafiti kwenye vituo vya kilimo, kutokomeza ndorobo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika nchi yetu haimiliki teknolojia ya kuzalisha nishati ya nyuklia lakini katika ardhi yetu kuna uwezekano wa kuwepo madini kama *uranium* ambayo yanaweza kutumika kuzalisha nishati ya nyuklia kwa ajili ya matumizi ya amani na salama. Hivyo mikataba hii na hitifaki zake zitasaidia sana Serikali kupanga mipango yake ya maendeleo katika eneo hili la matumizi ya nishati ya nyuklia.

Mheshimiwa Spika vile vile kamati yangu iliona umuhimu wa Bunge kuridhia mikataba hii kwa kutambua kwamba katika matumizi ya teknolojia ya nyuklia ajali yaweza kutokea na hivyo nchi yetu ikalazimika kutoa taarifa ya ajali hiyo mapema iwezekanavyo kwenye shirika la nguvu za atomiki duniani na kupata msaada wa kukabiliana na ajali hiyo haraka chini ya masharti ya *Convention On Assistance In Case Of A Nuclear Accident Or Radiological Emergency.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo hapo juu kamati yangu inamuunga mkono hoja ya Serikali ya kuomba Bunge kuridhia mikataba ya Kimataifa mitano inayohusu matumizi salama na ya amani nishati inayotokana na teknolojia ya nyuklia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kuridhia mikataba hii kamati inatoa ushauri ufuatao: -

1. Kwa vile nchi yetu inatumia teknolojia na nishati ya nyuklia kwa amani tu kama vile kwenye *X-rays,* tiba ya saratani, utafiti wa kisayansi mfano utokomiezaji wa ndorobo na kadhalika, ni vema Serikali ihakikishe kuwa vifaa vyote na mabaki yote ya teknolojia ya nyuklia ambayo wataalam wamehakikisha kuwa yana mionzi hatari kwa viumbe hai yahifadhiwe katika sehemu maalum zilizoidhinishwa na mamlaka zinazohusika ili kuondoa uwezekano wa ajali itakayotokana na matumizi ya vifaa hivyo.

2. Kamati inashauri Serikali kuchukua tahadhari na kuwa makini sana katika kuagiza vifaa vinavyotumia nishati ya nyuklia na kuona kuwa teknolojia inayoingiza nchini ni ile inayokubalika na kutambuliwa kuwa ni salama na ya kisasa vinginevyo nchi yetu itageuzwa kuwa dampo la vifaa hatari na vilivyopitwa na wakati.

3. Baada ya Bunge kuridhia mikataba hii Serikali iwasiliane na makao makuu ya shirika la nguvu za atomiki duniani ili kuwezesha nchi yetu kupata haki zote zinazotokana na kuridhia mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya kamati ya huduma za jamii naunga mkono hoja ya kuridhia mikataba mitano ya Kimataifa inayohusu matumizi salama na ya amani katika kutumia nishati ya nyuklia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU (MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI):** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa maoni ya kambi ya Upinzani kuhusu maazimio ya Bunge ya kuridhia Mikataba na itifaki za Kimataifa kuhusika.

1. Mkataba wa kutokomeza au kutoendeleza matumizi ya silaha za nyuklia;

2. Kutumia nishati ya nyuklia kwa shughuli za amani;

3. Itifaki ya nyongeza kwa ajili ya usimamizi madhubuti wa *Safeguards Agreement;*

4. Utoaji wa taarifa mapema juu ya ajali ya nyuklia pamoja na misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia na dharura ya ki-radiolojia.

Mheshimiwa Spika sasa nitapenda kupitia mkataba au itifaki moja moja na baadaye kuzijadili kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika kambi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono Azimio la Bunge la kuridhia mkataba wa Kimataifa unaohusu azma ya kutokomeza au kutoendeleza matumizi ya silaha za nyuklia. *(Non-Proliferation Of Nuclear Weapons Treaty).* Kambi inaunga mkono Azimio hili kwa kutilia maanani kuwa: -

1. Mkataba husika unazitaka nchi zilizotia saini mkataba huo na pia zinazomiliki silaha za nyuklia kutoruhusu kuhamisha silaha hizo kwenda nchi nyingine kwa namna yoyote ile na pia kutoshawishi au kutosaidia nchi zisizo na silaha za nyuklia kutengeneza au kupata silaha hizo.

2. Mkataba huo unazitaka nchi zisizo miliki silaha za nyuklia kutopokea silaha hizo au vifaa vingine vinavyohusika na utengenezaji wa silaha za nyuklia.

3. Mkataba unaziwajibisha nchi zilizosaini huo kusaini mkataba wa *Safeguards* kati yake na shirika la nguvu za atomiki duniani. Kulingana na katiba inayounda shirika hilo.

4. Kambi ya Upinzani inatilia maanani sera ya taifa ya Sayansi, teknolojia ya mwaka 1996 inayoelekeza matumizi salama ya amani ya nishati ya nyuklia katika sekta mbalimbali za maendeleo kama vile elimu, kilimo, afya, nishati, udhibiti na mionzi aionyesha.

5. Tunatilia maanani kuwa tayari Tanzania ni mwanachama wa mkataba mwingine wa *The Africa Nuclear Free Zone Treaty, The Perina Treaty.*

6. Kwamba Tanzania tayari kupitia Bunge hili imekwisha pitisha Muswada wa *The Atomic Energy Act , 2003* mnamo *April, 2003.*

7. Na muhimu zaidi kambi ya Upinzani inaamini kuwa utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia:-

1) Hayasaidii kuondoa umaskini duniani;

2) Hayasaidii kuondoa magonjwa duniani;
3) Hayasaidii kuondoa njaa na ukame duniani kinyume chake mashindano hayo yanasaidia kuzidisha umaskini, ufukara, hofu, mashaka na upotevu wa amani duniani na ni kutokana na hayo yote kambi ya Upinzani inaunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kambi ya Upinzani inaelewa kabisa kuwa suala la kuwa au kutokuwa na utengenezaji wa silaha za nyuklia katika nchi mbalimbali duniani inazo sura mbili za kiuchumi na kisiasa. Hoja hizi nitazijadili katika hitimisho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kambi ya Upinzani imekwisha kukubali Azimio la kuridhia mkataba wa kutokomeza au kutengeneza matumizi ya silaha za nyuklia basi kambi vile vile inaunga mkono mkataba wa Kimataifa unaokusudia kutumia nishati ya nyuklia kwa shughuli za amani na si utengenezaji wa silaha za nyuklia *(Safeguard Agreement).*

Mheshimiwa Spika, vile vile kambi ya Upinzani inaunga mkono Azimio la kuridhia itifaki *The Additional Protocol* ya Kimataifa ya usimamizi madhubuti wa *Safeguards Agreement.* Kwa kuwa itifaki hii ni nyongeza ya mkataba wa kwanza yaani *the Safeguard Agreement* na kwa vile itifaki inakusudia kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia na kukagua shughuli zote za kinyuklia zilizoainishwa na zile zisizo ainishwa ni *declared and undeclared nuclear material / activities* ili kuhakikisha kwamba hazitumiki kwa madhumuni ya kutengeneza silaha za nyuklia.

Mheshimiwa Spika kwa vile kambi ya Upinzani inaelewa kwamba pamoja na kuwepo na mikataba na itifaki za Kimataifa kuzuia utengenezaji wa silaha za nyuklia bado kuna nchi korofi zinazoendelea kutengeneza silaha hizo na zingine zikijaribu kupata teknolojia na madini ya kutengeneza silaha hizo, hivyo ni vema itifaki hii ya nyongeza inajaribu kuzuia ili usiendelee kutokea.

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya kambi ya Upinzani naunga mkono Azimio la Bunge la kuridhia mkataba wa Kimataifa unaohusu utoaji taarifa mapema juu ya ajali za nyuklia *Convention On Early Notification Over A Nuclear Accident.* Ina jaribu kuzuia hilo lisiendelee kutokea.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naunga mkono Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Utoaji Taarifa mapema juu ya Ajali za Nyuklia *(Convention on Early Notification of a Nuclear Accident).* Inaeleweka kuwa shughuli za matumizi ya nishati ya nyuklia imeongezeka sana hasa katika shughuli za afya mahospitalini katika kutibu na kuchunguza magonjwa viwanda, elimu kilimo, utafiti na vinu vya kuzalisha nguvu za umeme. Pia inaeleweka kuwa zimewahi kutokea ajali mbaya za mitambo ya nyuklia kama ilivyotokea huko Chinaberry Urusi mwaka 1986. Kwa vile ajali hizo zikitokea zina athari kwa binadamu, wanyama, mimea na mazingira katika nchi ajali ilikotokea na hata kwa nchi za jirani. Ni kwa mantiki hiyo Kambi ya Upinzani inaunga mkono Azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaunga mkono Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Misaada ya Kushughulikia Ajali za Nyuklia au Dharura ya Kiradiolojia *(Convention on Assistance in the Case of a Nuclear Accident or Radiological Emergency).* Madhumuni ya Mkataba huu ni kuhakikisha kuwa nchi zilizotia saini Mkataba huu zinashirikiana miongoni mwao na vile vile kushirikiana na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani ili kuwezeshwa upatikanaji wa msaada kwa kushughulikia ajali au dharura za Kiradiolojia kwa madhumuni ya kupunguza madhara

yake na hivyo kulinda maisha ya binadamu mali na mazingira. Tunaunga mkono madhumuni hayo.

Mheshimiwa Spika, wakati nikianza kuunga mkono Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Azma ya Kutokomeza au Kuzuia Uenezaji wa Silaha za Nyuklia, nilisema suala la kutengeneza au kutotengeneza silaha za nyuklia lina sura mbili za kiuchumi na kisiasa.
Kambi ya Upinzani imeunga mkono Maazimio ya Kuridhia Mikataba hii si kwa sababu ya kuunga kila kitu mkono kwa falsafa ipite. Tumeunga mkono kwa vile sisi katika Kambi ya Upinzani tunaamini katika kuendesha siasa za nchi au Umoja wa Mataifa kwa nguvu za hoja na si kwa nguvu za nguvu.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa *Non Proliferation Treaty* mwaka 1998 kuna nchi hazikutia saini Mkataba huo. Nchi hizo ni kama India na Pakistan ambazo zote zimeendelea kutengeneza na kufanya majaribio ya silaha za nyuklia. Pia kuna nchi ambazo zimetia sahihi mkataba lakini zimekuwa zikijaribu kutengeneza silaha za nyuklia kama vile Korea Kaskazini na Iran.

Tatu, hata zile nchi zilizokwishakuwa na silaha hizo kama vile Marekani, Urusi, Uchina, Ufaransa na Uingereza bado hazijaacha kutengeneza silaha bora zaidi kila kukicha. Ni kutokana na hayo kukawa na hiyo hoja ya kuwepo na masuala ya siasa katika kuendeleza mashindano ya utengenezaji wa silaha hizo. Pengine nchi kama Iran na Korea Kaskazini zinafanya hivyo kwa sababu za kiuchumi na kiulinzi. Sasa mtu anaweza kujiuliza kama mataifa makubwa kama Marekani yanatumia nafasi ya kuwa na silaha za nyuklia na zile za kisasa kabisa kupuuza maamuzi ya Umoja wa Mataifa je, misingi ya Mataifa mengine yenye uchumi mzuri kuvumilia na kulinda misingi ya kuheshimu uamuzi wa Umoja wa Mataifa itatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, nani anaweza kutabiri kwa usahihi kuwa katika miaka 50 ijayo baada ya nchi nyingine kuwa zimekuza uchumi wao kiasi cha kuipiku Marekani hawatashawishika kuanza tena ari ya kutaka kutengeneza silaha za nyuklia. Ni kutokana na hofu ya hoja hizo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ya Tanzania kwa nafasi yake ya kuwa mwanachama wa muda katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kuanzisha mjadala wa kushinikiza mataifa yenye silaha za nyuklia waziharibu bila masharti wala bila kiburi.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo ule msemo kuwa Mataifa yenye kuwa tayari na silaha hizo yawe nazo tu na yale yasiyokuwa nazo yasiwe nazo eti kwa vile zinaweza kuangukia kwenye mikono ya mataifa yanayoongozwa na viongozi wasio na busara. Si kweli! Busara ya kweli ni ile aliyotuachia Yesu Kristo kuwa, "*Do and have others do as you do"*. Tunaomba Bunge liliridhie maangalizo haya lakini liweke angalizo na kupaza sauti kwamba mataifa yenye silaha za nyuklia waziharibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. PHILLIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu wa mawazo katika mikataba hii muhimu ambayo tunataka kuiridhia.

Mheshimiwa Spika, mikataba ambayo iko mbele yetu hasa Mkataba huu wa Kutokomeza au Kuzuia Uenezaji wa Matumizi ya Silaha za Nyuklia ni muhimu sana. Kwa vile Mikataba mingine inawezeshwa tu, Mkataba huu uweze ukafanya kazi ipasavyo. Mimi katika kujadili mikataba hii nitajielekeza kwenye Mkataba huu wa awali (*Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty - NPT)*

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ulitungwa na Umoja wa Mataifa kutoka miaka ya 1960 na leo mwaka wa 2004 ni muda mrefu sana. Baadaye nitauliza ni kwa nini nchi yetu imechelewa sana kuridhia Mkataba huu. Tanzania ni nchi ambayo inathamini na imekuwa mfano wa kudumisha amani duniani. Mkataba wa matumizi ya silaha za nyuklia ni Mkataba mmojawapo wa kudhibiti amani duniani. Hivyo baadaye pengine Waziri atuelezee ni kwa nini hasa kwa miaka karibu 30 na kitu hatujaweza kuridhia Mkataba huo muhimu.

Inawezekana Mkataba huu ikiwa ni Mikataba ya dharura iliyoletwa Bungeni kwako na kutaka kuridhiwa katika Bunge ni kwa sababu kwa vile Tanzania imechaguliwa kuwa mwanachama wa muda wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Kazi kubwa ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa katika nyakati hizi ni kusimamia amani duniani na kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Nguvu za Atomiki, kusimamia matumizi ya silaha za nyuklia hasa kusimamia utengenezaji na kupiga marufuku utengenezaji wake. Kama ndiyo hivyo basi nampongeza Mheshimiwa Rais na waliohusika kufanya kampeni hadi Tanzania ikachaguliwa kuwa mwanachama kwa muda wa miaka miwili ijayo katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Hii ni heshima kubwa sana na tutashuhudia siku za karibuni kwa viongozi mbalimbali kutoka kote duniani wakija Dar es Salaam kushauriana kuhusu masuala ya amani duniani. Tumekwishaona kwa mara ya kwanza ujumbe kutoka Morocco na baadaye mwezi huu kutakuwa na mkutano mkubwa wa masuala ya amani katika Maziwa Makuu, ambao kwa mara ya kwanza utahudhuriwa na Mheshimiwa Koffi Anan, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa pamoja na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, ambaye pia ni Rais wa Nigeria, Mheshimiwa Obasanjo na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, heshima hii nayo lazima itakuwa na gharama yake. Serikali kwa jumla bila shaka imejiwekea mikakati ya kugharamia heshima hii. Kwa wale ambao wameweza kufika Umoja wa Mataifa kazi ya Baraza la Usalama ni saa 24, miezi 12 kwa mwaka na muda wote. Kwa hiyo, nchi ambayo ni Mjumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lazima iwe na watumishi wengi sana wa ngazi ya Ubalozi na ngazi za chini. Hivyo, bila shaka Ubalozi wetu ulioko Umoja wa Mataifa sasa utaongezeka maradufu. Kutakuwa na gharama ambazo pengine zimefichika kama kuwapokea wageni hawa, kuwa mwenyeji wa Mikutano mikubwa kama hii.

Mheshimiwa Spika, nikirejea kwenye Mkataba huu ambao tunauridhia kwamba kuna lile suala la kwa nini tumechelewa muda huu wote, kwa sababu ni Mkataba ambao

kinyume na matarajio yetu, mkataba wenye matarajio makubwa kwetu sisi kwanza kwa kunufaika na programu za Shirika la Umoja wa Mataifa la silaha za Atomiki (*International Atomic Energy Agency*) ambayo makao yake Makuu yako Vienna. Lakini pia kuridhia Mkataba huu mapema ni kielelezo cha kuunga amani na wapenda amani duniani. Kutokupiga vita matumizi ya silaha za nyuklia ni kuachia mustakabali wa maisha yetu na uhai wa binadamu na mimea katika watu ambao pengine wasingeweza kusemea matakwa yetu. Kwa hiyo, ni sababu moja kwa nini tumechelewa muda huu wote.

Lakini pia kutokuridhia Mkataba huu kwa muda wote kumekuwa na athari kubwa katika nchi yetu na watu wake. Fani hii ya nguvu za Atomiki ni fani ambayo iko nyuma sana katika nchi yetu kuliko nchi zingine hata majirani kiasi ambapo hata wataalamu wetu waliobobea katika eneo hili hawawezi kurejea nchini kwa sababu hawawezi kutumia taaluma yao ipasavyo kwa sababu hakuna taasisi zilizobobea katika eneo hili. Nchi maskini kama sisi kama Bangladesh ilishawahi kuwa na kituo kikubwa cha nguvu za Atomiki (*Atomic Energy Centre*) toka miaka ya 1970 na wataalamu wengi wa Bangladesh wamerejea kutoka Ulaya na Amerika, kwa hiyo, tuna wa kwetu.

Pengine si vibaya kusema kwamba aliyekuwa Waziri Kiongozi wa Zanzibar, Mheshimiwa Bilal ni mtaalam mmoja aliyebobea katika eneo hili. Nadhani hatapenda kwenda Ulaya kufanya kazi yake ya kufundisha. Ndiyo hali iliyotufikisha hapo na mimi nadhani ni mojawapo ya chanzo au sababu ya Tanzania kutokujihusisha katika eneo hili la nguvu za atomiki. Taasisi tuliyonayo pale Arusha ni taasisi ndogo sana ya kuratibu shughuli ndogo ndogo kama *X-ray* na kadhalika. Sasa wakati umefika basi kama nchi ambayo katika nchi chache sana duniani ni Mjumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa na kituo kikubwa ambacho kinazalisha nishati ya nyuklia kwa matumizi ya maendeleo na kadhalika.

Nitashangaa sana tutajihusishaje kikamilifu kama wajumbe wa Baraza la Usalama kuongelea kwa kina kuanzia sasa hadi miaka ijayo masuala magumu ya Kashmir. Kwa hiyo, sasa ndio wajibu wetu kama wajumbe wa Baraza la Usalama, masuala ya Iran, Korea Kaskazini. Kama wataalamu wetu watashauri viongozi wakitafuta suluhu ya amani duniani kwa sababu hii ni zaidi ya siasa ya kawaida. Maana yake ni nini? Amerika inapotupia lawama kubwa sana Iran na Korea Kaskazini kwa sasa, tukichaguliwa kama viongozi wa kutatua suala la Korea Kaskazini na suala la Iran tutakuwa na *resource persons* wa aina gani? Nina hakika itakuwa ni wajibu kupeleka haraka iwezekanavyo pengine wanajeshi maeneo kama Dafur. Tunaweza kuongelea pengine kwa ufasaha zaidi masuala ya Palestina lakini kama wanachama wa Baraza la Usalama tunaweza kuongelea kwa kina, kwa undani na kwa taaluma zaidi masuala ya matumizi ya nguvu ya nyuklia kule Iran au Korea ya Kaskazini au Kashmir kwa maana ya mashindano ya matumizi ya nguvu ya nyuklia kati ya India na Pakistan.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi mimi nataka kusema kwamba pamoja na kuchelewa kuridhia Mkataba huu basi sasa tuwe na mikakati na programu ya kuendeleza nishati hii katika malengo ya amani na ya maendeleo na katika malengo ya Tanzania kuwa na usemi kutumia nafasi yake hii ya kuwa mwanachama wa Baraza la Usalama

kwa ukamilifu zaidi na kwa Taifa. Hivyo basi siyo tunaongelea suala hili kwa ukamilifu kwa maana ya siasa tu lakini katika hali halisi iwe kwa manufaa ya kimaendeleo ambayo nchi yetu itapata toka sasa kwa kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika kuridhia Maazimio matano yaliyotolewa na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.. Serikali imevunja ukimya, baada ya muda mrefu miaka 30 kwa jumla Mikataba yote mitano ambayo ilikuwa tunaridhia leo katika Bunge lako Tukufu ni juhudi za Serikali katika kuwa makini kuangalia kwa makini Maazimio kama haya na sheria kama hizi na Mikataba kama hii ya kisayansi na kuwa makini kuangalia matokeo ya wenzetu na matokeo yaliyotokea katika nchi zilizoendelea. Kwa sababu haya ni Maazimio ya kisayansi kwani nyuklia ni nguvu si kitu. Kwa sababu nguvu haionekani huwa inahimili tu. Kwa hiyo hutoweka na vile vile hujitokeza. Kujitokeza kwake hupimwa kwa vipimo vya usikivu havipimwi kwa ujazo wala urefu. Kwa hiyo *it is not sensible.* Kwa hiyo, mara nyingi nguvu ina *power of feeling,* inakuwa *greater* kuliko *power of reasoning.* Popote utakapokwenda nguvu huenda kwa kuelekezwa na chombo tunachokituma. Hivyo basi hakififikirii nguvu iendako ila huelekezwa na kutumwa kuendako huko, hivyo kuweko na vyombo vya udhibiti vya dunia ili kudhibiti hali hii. Ndiyo maana katika masuala haya ya nyuklia kuna mambo matano, *Bomb Dropping (1945), 1st Chain Reaction, (1944), Nuclear Regulatory Commission, (1982), Power Production (1981), Accidents* hii ni matokeo tu haina mwaka na *Chronology (1999).*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ni kwamba Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria mwaka 2003 ya Nguvu ya Atomiki. Hatua hii ni mfululizo tu wa utekelezaji wa kuungana na dunia jinsi ya kuepusha vitu vilivyoko duniani, viumbe hai kama binadamu, wanyama, mimea na vitu vingine. Tukiangalia nchi yetu katika matumizi ya nguvu na matumizi ya vitu muhimu ambavyo wenzetu wako mbali, kwa mfano, tunavuta maji kwa nguvu za mserereko, mafuta, umeme, upepo. Wenzetu wanatumia nyuklia. Umeme tunatumia *hydro* na *Songas,* wenzetu wanatumia *nuclear.* Wakati uuaji wa wadudu kwa mfano tunapohasi wadudu kama mbung’o tunatumia *pesticides* lakini sasa hivi wenzetu wanatumia nyuklia. Kwa upande wa injini na mitambo tunatumia mafuta na umeme wakati wenzetu wanatumia nyuklia asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naitahadharisha Serikali kuwa baada ya kuridhia Mikataba hii hatuna ubavu wa kuhimili na kupima uwezo, ujazo au kiasi cha nyuklia mionzi katika nchi yetu. Lakini tuna uwezo wa kutumia nchi ambayo tunaungana nazo ili tuweze kupima. Kwa sababu ukiangalia Nchi Zinazoendelea duniani kuna matukio ya madhara mazito kadhaa ambayo yalijitokeza. Ilinipa wasi wasi kwa kuwa tutahilimi vipi vitu kama hivi wakati wenzetu walioendelea wamepata madhara? Lakini kumbe sisi hatutakuwa na *reserve* za nyuklia na mitambo ya nguvu za nyuklia *production* tutakuwa na watumiaji wa vifaa kadhaa ambavyo vilikuwa vinadhibitiwa na kuangaliwa kwa makini na Serikali yetu visilete athari kama ilivyotokea katika maeneo ambayo nitawatajia.

Kwa mfano nchi kama Poland Oktoba tarehe 5, 1966 kuna *cooling system* ya mtambo wa nyuklia ulitayarishwa vibaya (*mis-handling*) karibu wafanyakazi 25 waliathirika. Tarehe 7 Oktoba, 1957 kule Liverpool ilitokea *radiation* ya mionzi na kusababisha wafanyakazi 39 wafariki. Japan Kaskazini ya Mashariki ya Tokyo tarehe 8 Oktoba, 1986 kijiji cha Tokaimre *uranium* imetoa mionzi mingi kupindukia ilisababisha watu 165,000 kuhama, na 22 kufa. Japan Tsunja tarehe 26 Aprili, 1981 wakati wanafanya ukarabati wa *nuclear plant* wafanyakazi 100 waliathirika. Sasa hiyo ilikuwa inadhihirisha wazi kwamba Nchi Zilizoendelea zinazotumia nguvu za aina hii vilevile wanaathirika kutokana na *reactions* za vitu hivyo. Kwa hiyo, Udhibiti wake wa mitambo ni hatari kweli kweli. Hiyo ni mifano michache tu, ipo mingi. Hivyo basi nchi iwe makini kwa kutumia wataalam hawa niliowataja. Wahifadhi maeneo ya *reactions* ya ile kemikali kama *uranium* na vitu vingine, mitambo ya *X-ray* kwa mfano *Ocean Road* wanapofanya ile mitambo ya kutibu saratani wangeweka maeneo ya kutoa onyo kwa watu ambao wasisogelee maeneo hayo au wasitembee maeneo hayo. Kitu kimoja ni kwamba kuunda *Commission* ndio kunakuwa na taasisi ndogo ya wataalamu waliobobea siyo waliozoea kwa sababu hatuna chuo cha uzoefu. Basi wale waliobobea watatusaidia katika hadidu za rejea katika kuangalia mambo hayo ama sivyo tutaweza kupata matatizo. Kwa hiyo, nyuklia ni nguvu si kitu na nguvu ziko *sensitive* siyo *sensible.* Hivyo, hazifikirii nguvu ziende wapi, zinapelekwa huko zinakoelekezwa. Kwa hiyo basi athari zinazotokea ni athari kwa Watanzania. Naomba tuwe wazi kwa hili na naunga mkono Mkataba huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kubwa kwa michango iliyotolewa hapa Bungeni. Kwanza, kwa Mwenyekiti wa Huduma za Jamii na Kamati yake kuhusu Maazimio haya. Pili, kutoka kwenye Kambi ya Upinzani ambayo imeweka bayana kabisa. Maelezo mazuri kabisa yaliyotolewa kuhusu Maazimio yetu wananchi wameyasikia. Vile vile wachangiaji, Mheshimiwa Marmo na Mheshimiwa Pawa tunawashukuru sana kwa michango yao mizuri ambayo wameweka tahadhari. Mheshimiwa Pawa *I suppose* nguvu *power* ambayo yenyewe siyo *sensible*. Ni *sensitive* lakini *not sensible*. Yote haya tunayazingatia.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetoa maoni na wasi wasi na ikaomba kuitaka Serikali ichukue tahadhari katika matumizi haya ya nishati katika utekelezaji wa Mikataba hii, ili kupunguza uwezekano wa kutokea silaha za nyuklia. Vile vile suala hili limezungumziwa na Mheshimiwa Pawa, mabaki ya vyanzo vya mionzi, matumizi ya vyombo hivyo. Serikali imejenga maabara ya kuhifadhia mabaki ya vyanzo vya mionzi inaitwa *Radiactive West Management facilities* katika eneo la Njiro, Korona, Arusha. Jengo hilo lilijengwa kwa kuzingatia kanuni na viwango vinavyokubalika kimataifa . Bahati nzuri Kamati ya Bunge iliwahi kufika na kutembelea maabara hiyo. Maabara hiyo itazidi kupanuliwa ili iweze kukidhi mahitaji yetu.

Vile vile kwa kuingia Mikataba hii na kuridhia, kama tulivyoeleza katika maelezo yetu ambayo tumeyaleta mbele ya Bunge hili ndiyo tutapata manufaa ya kusaidiwa na wenzetu ambao wana uwezo. Shirika la Atomiki Duniani na asasi

mbalimbali za kimataifa zinaweza kutusaidia kwa sababu zitakuwa zimeweka imani kwamba tumeingia katika Mkataba, kwamba tunaweza kulinda matumizi halali ya amani katika nguvu za Atomiki. Serikali itaendelea kuwa makini kwa kuhakikisha kwamba katika kuagiza vifaa vyote vinavyotumia nishati ya nyuklia na teknolojia hii vinakubalika na kutambuliwa kuwa ni salama na ya kisasa na kwa matumizi ya amani ili kuepusha Taifa kugeuzwa kuwa *dampo* kwa vifaa hatari vinavyotumia nishati za nyuklia. Hii tuko macho kabisa tutailinda nchi yetu isiwe *dampo.*

Mheshimiwa Spika, wataalamu toka Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki hufanya ukaguzi na utoaji hati kwa watumiaji vifaa vinavyotumia nishati na nyuklia kwa mfano mashine za *X-ray* hospitalini. Matumizi ambayo yameleta manufaa katika Tanzania ni matumizi ya nishati ya nyuklia katika kuondoa hatari ya ndorobo katika nchi yetu hasa katika visiwa vya Zanzibar, Pemba pamoja na Mafia. Tunataka tuendelee na utaratibu huo tujaribu sehemu kubwa tuingie hapo Bagamoyo na utaalamu wetu umekubalika na kuchukuliwa na nchi zingine. Sasa hivi ndorobo ambao tunao huko Tanga wanapelekwa nje kwenda Ethiopia ambapo ni hatari kubwa wale ng'ombe wasiwe wanapata hatari ya kutokuwa na manufaa kwa wananchi wa Ethiopia. Wana ng'ombe karibu 35,000,000 katika nchi ya Ethiopia lakini hawana faida kwa sababu ya matatizo ya mbung'o.

Mimi nilipotembelea *The Atomic Energy Agency* ya Dunia pale Vienna Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hili aliniuliza nyinyi kule Afrika mbona hamtilii maanani sana ng'ombe wenu. Ng'ombe wenu katika mipango ya maendeleo hamtilii maanani kuondoa ndorobo kwa kutumia *atomic energy.* Kwa hiyo, akaangalia mbona hamna mpango kamilifu wa sisi kuwasaidieni ili muweze kuondoa ndorobo. Mimi nikaitikia wito huo tumeweka mpango madhubuti wa kuweza kuondoa ndorobo katika nchi yetu na nchi jirani.

Jambo lingine ambalo tulijadili na huyu Mkurugenzi ni uwezekano ambao ingawa hatujui sasa uwezekano uko kiasi gani, lakini upo. Kwa kutumia nishati hiyo hiyo, nguvu hizo hizo zikawa *sensitive.* Hii ya mdudu mdogo sana anaitwa mbu ambaye ni hatari sana. Kama ndorobo hapa ni aina ya nzi ameweza kushughulikiwa hivyo watafiti wetu wa afya wanajitahidi kuona kama mbu wanashughulikiwa kwa njia hiyo hiyo akapungua na tukatoa adha ya mauaji makubwa ambayo yanatokea duniani kuliko hata bomu la Atomiki kwa malaria, hiyo tunafikiria.

Baada ya Bunge kuridhia Mikataba hii, Jumuiya ya Kimataifa itaitambua nchi yetu kwamba haina agenda ya siri ya kutengeneza silaha za nyuklia wala kupokea wala kununua au kuiwezesha nchi yetu kupewa misaada ama pia kuiendeleza teknolojia hii kwa madhumuni ya kushambulia watu au kuwa na nguvu za mabomu ya kuweza kudhuru wanadamu au mimea au mali yoyote ile. Kwa hiyo, haya ndiyo maelezo kwa ile hoja ya Kamati ya Huduma za Jamii.

Kwa upande wa Upinzani sina mengi ya kusema ila kuwashukuru sana kwa kuboresha ile hoja yetu. Mimi kama Waziri na Mbunge wa Bunge lako Tukufu hapa nimefurahi sana kwamba wametoa kwa maandishi tena kwa usahihi na ufanisi mkubwa.

Nashukuru sana tutayafanyia kazi. Kwa kuwa sasa tumeweza kuingia katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ambalo ndio hasa Baraza Tendaji linalodhibiti hali ya amani duniani shinikizo kubwa kwa nchi kubwa ambazo zimeingia na ambazo zitaingia kwenye Mkataba huu tunaweza kulifanya sasa, tumepata nafasi hiyo. Tutatumia *moral power* tuliyonayo maana yake hatuna nguvu nyingine *a moral power* na ushawishi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nguvu hii inajitokeza sana siku hizi kuliko zamani. Zamani waliona kwamba wakubwa wanaweza kutenda wapendavyo lakini sasa kuna shinikizo la watu wengi likiwekwa pamoja katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na hasa ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, nadhani hawa wakubwa watatusikia. Hiyo sheria inabadilika pole pole ya kuwasikiliza wale wadogo. Tanzania kuingia kule kwa imani kubwa hiyo ya Mataifa yote tutaitumia imani hiyo kama *moral power* ya kuweza kusaidia kuwashinikiza hao ambao hawataki kufuata utaratibu huu ambao dunia imejiwekea. *(Makofi)*

Swali ambalo Mheshimiwa Marmo na Mheshimiwa Pawa waliuliza maana yake mengine yanafanana na haya, waliuliza ni kwa nini tulichukua muda kiasi hicho? Majibu yangu ni kwamba kwa sababu suala lenyewe ni zito, ni nyeti siyo la kushtukia unaingia tu. Mikataba mingi unaweza kuingia hutafakari sawa sawa, ukawa sasa wewe umetumiwa tu kama ni sehemu tu ya matumizi ya watu wengine na tulipojitawala Mwalimu Nyerere alikuwa makini sana juu ya Mikataba, kwamba huingii tu Mikataba hivi hivi tu bila kufikiria. Wakati ule Mikataba ilikuwa inawekwa na hasa inapoanzishwa na wakubwa kulikuwa ni halali, kusita na kuangalia kwamba ni kwa manufaa ya nani na hasa wao walipojitenga kwamba kuna wale ambao watakuwa na nguvu. Nguvu hizo ni zao watakuwa nazo na wana akili ya kuzidhibiti na wengine ambao hawana akili ya kuzidhibiti. Wakati huo ni bado mimi naungana na Serikali zilizotangulia hasa Mwalimu na zingine hizi kwamba ilikuwa ni busara kufikiria na kutafakari kwa makini kama tuna uwezo. Unaweza hata ukajiuliza kwa nini hatuchimbi mafuta ya petroli, kwa nini hatuchimbi *uranium* na tunayo sasa hivi? Kwa sababu uwezo wa kudhibiti vitendo hivyo hatuna. Tutakapoupata hii mali yetu tutaitumia tu. *Uranium* tunayo ya kutosha hapa, *copper* tunayo ya kutosha, lakini tukianza kuichimba itatuletea madhara na adha kubwa zaidi kwa sababu huwezi kudhibiti. Sasa kwa elimu na kwa technolojia tuliyonayo na hatua ya maendeleo ya taifa letu nadhani umefika wakati sasa kwamba tuingie huko, ndiyo jibu ninaloweza kutoa. Hatujachelewa. *(Makofi)*

Kwa kuingia katika Mikataba hii ndiyo tutatafuta uwezo na tumeanza kutafuta uwezo huo. Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Mataifa ya *Atomic* yuko tayari kabisa kutupatia uwezo wa kufundisha watalaam wetu. Watalaam wetu tulionao wanaweza kurudi wakatusaidia. Tuko tayari na maandalizi yapo mbioni pale Chuo cha Dar es salaam kuanzisha somo hilo la *Neuclear Physics* na la *Neuclear Energy* na katika Taasisi mbalimbali ambazo zitakazoanzishwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatujachelewa na ni mtiririko tu wa matukio ambayo yaliandaliwa hata kabla hatujaingia katika Baraza hili la Usalama la Kimataifa. Mwaka 2003 Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria ya *Atomic,* tulikuwa bado hatujawa Wajumbe kwenye Baraza

hilo. Yalikuwa ni maandalizi mazuri. Hivyo, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako tukufu kwa kuturuhusu kuleta maazimio haya na kukubali kuyaridhia.

Kwa hiyo, natoa hoja sasa kwamba Maazimio haya ambayo yamewekwa mbele ya Bunge lako Tukufu sasa Bunge liyaridhie.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Maazimio haya matano yafuatayo yaridhiwe na Bunge.

Mkataba wa Kimataifa unaohusu Azma ya Kutokomeza au kuzuia Uenezaji wa Silaha za Nyuklia *(Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty - NPT).*

Mkataba wa Kimataifa unaokusudia kutumia Nishati ya Nyuklia kwa shughuli za amani tu na siyo katika Utengenezaji wa silaha za Nyuklia *(Safeguards Agreements).*

Azimio la Kuridhia Mkataba unaohusu Miswadaa ya Kushughulikia Ajali za Nyuklia au Dharura ya Kiradiolojia (*Convention on Assistance in the Case of a Nuclear Accident or Radiological Emergency).*

Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Utoaji Taarifa Mapema juu ya Ajali ya Nyuklia *(Convention on Early Notification of a Nuclear Accident).*

Azimio la Kuridhia Itifaki (*Additional Protocol)* ya Kimataifa ya Usimamizi Madhubuti wa *Safeguard Agreements.*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mikataba na Maazimio ya Suala la Nyuklia yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa ulihitajika uamuzi wa Bunge na uamuzi bora tumefanya kwa pamoja kwa Maazimio yote matano. Sasa Bunge limekubali kuridhia Maazimio yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Waheshimiwa Wabunge, *Order Paper* ya leo ilitengenezwa kwa makusudi ili kikao cha leo kimalizike kabla ya saa saba. Kwa hiyo, tumefanikiwa lengo hilo. Hivyo, sasa leo mchana tutakuwa na *bonus*. Mimi sasa naliahirisha Bunge mpaka kesho ili mchana tufanye kazi nyingine. Baada ya maelezo hayo sasa naahirisha Bunge, mpaka kesho Asubuhi Saa Tatu. *(Makofi)*

*(Saa 06.03 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa*
*Tarehe 5 Novemba, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*